

# *WAKATI WA*

## *KANISA LA SMIRNA*

 Baba yetu Mtukufu sana, tuna furaha sana usiku wa leo kujua ya kwamba katika utu wetu tunao Uzima usiopatikana na mauti. Ule Uzima wa Mungu wetu uliogawanywa kwa ndimi za moto na kuketi juu ya kila mmoja wao, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka. Ee Baba, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwamba Wewe ulijigawa Mwenyewe mionganini mwa Kanisa. Si ajabu Bwana wetu alisema, "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Jinsi Mungu wa Mbinguni anavyoishi mionganini mwa watu Wake! "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari." Kote katika kila wakati wa kanisa Wewe ungekuwa hapa, ye ye yule jana, leo, na hata milele, nasi tungekujua kwa kazi uzitendazo. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

<sup>2</sup> Bwana, tukiona—tukiona upeo wa nyakati zote, wakati uko karibu kwisha na Umilele kuingia. Baba Mungu, tuna furaha sana kujua ya kwamba tunaishi katika ile siku ya masalia leo hii; tukiyachunguza maisha yetu na tukiona aina ya malengo tuliyo nayo, nia tulizo nazo, na tukiona kwamba Roho Mtakatifu amechukua mamlaka. Mungu, jalia kila mitu katika Uwepo wa Kiungu usiku wa leo atambue nyakati hizi za kanisa tunazoishi na akimbie upesi kwa Bwana Yesu, kwa kuwa imeandikwa dhahiri sana, ya kwamba, "Jina la Bwana ni ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama."

<sup>3</sup> Ee Mungu, njoo usiku wa leo na kuutia utu wetu mafuta, Bwana. Walete wanaotangatanga, Ee Bwana, waliochanganyikiwa sana; waangalie maskini hawa kondoo, Bwana, hawajui la kuamini; kuna wito wa wachungaji kutoka kila mahali. Tunaomba, Baba, ya kwamba watamsikia yule Mchungaji mkuu wa kundi, Bwana Yesu, Roho Wake mkuu anene usiku wa leo, aseme "Mtoto Wangu, njoo Kwangu nami nitakupa Sabato, Raha inayokutia muhuri hata kwenye kikomo chako cha Milele." Sio kupeperushwa duniani tunapouona wakati ukiisha sasa. Tujalie, Baba. Nena kupitia kwa mnenaji, sikiliza kupitia kwa masikio ya hao wasikiao, kwa kuwa sisi sote tunasikiliza. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina. Mwawenza kuketi.

<sup>4</sup> Sasa, usiku wa leo tunasoma kwenye wakati wa pili wa kanisa. Ninaona wengi wao wakiandika muhtasari na kadhalika, na hiyo ndiyo sababu ninataka kulifanya hili dhahiri kila wakati.

<sup>5</sup> Sasa, wakati wa pili wa kanisa uliitwa wakati wa kanisa la Smirna. Nao ulichukua, Wakati wa Smirna, ulianza wakati ule ule Wakati wa Efeso ulipoisha. Wakati wa Efeso ulikuwa ni kutoka mwaka wa 55 A.D. hadi mwaka wa 170 A.D. Wakati wa Smirna ulilingia kwenye mwaka wa 170 na unaenda hadi 312. Kanisa hili ni kanisa lililoteswa; lile ambalo linavaa taji ya ufia imani, ni kanisa la dhiki. Na ahadi ya Mungu kwake, kwa Kanisa Teule ndani yake, ilikuwa ni kulipa taji ya Uzima.

<sup>6</sup> Kila kanisa likuwa na *nyota* iliyyoshikwa mkononi mwa Mungu, ambayo iliwakilisha “mjjumbe” kwa wakati huo wa kanisa. Yule mzuri sana ningaliweza kukumbuka alikuwa mjjumbe wa wakati wa kanisa la Efeso (kwa sababu Biblia haisemi hao ni nani) alikuwa ni Paulo; kwa sababu alilianzisha kanisa la Efeso naye alikuwa mhudumu wa wakati huo wa kanisa; ambaye aliletta Nuru Kanisani, ambapo Mtakatifu Yohana alilichukua kutoka hapo. Halafu Polycarp, na kuendelea... Polycarp, hasa, na kuendelea.

<sup>7</sup> Sasa, Wakati wa Smirna, ninaamini kwa ninii yote... ambavyo nimeweza kupata, alikuwa ni Ireneo. Na sasa nataka kuwapa sababu ya mimi kumchagua Ireneo badala ya Polycarp. Sasa, karibu makasisi wote wanataka kuwazia (na walimu wa Biblia) kwamba Malaika huyo alikuwa ni Polycarp. Polycarp alikuwa mwanafunzi wa Mtakatifu Yohana, hiyo ni kweli. Naye Polycarp alitia muhuri... a—alikuwa ni mfia imani, walimdunga kisu moja kwa moja moyoni na kumwua. Sasa, lakini yeze alikuwa ni mtu mashuhuri, mtu mwenye sifa, mtauwa, mzuri. Hapana shaka mmoja wa Wakristo hodari sana tulipata kuwa nao. Wala hakuna kitu ungaliweza kusema juu ya maisha yake.

<sup>8</sup> Sababu ya mimi kumchagua Ireneo: kwa sababu ninaamini kwamba Ireneo alikuwa karibu sana na Maandiko kuliko vile Polycarp alivyokuwa. Kwa sababu Polycarp kidogo aliegemea kwenye wazo la Kirumi la kuunda dhehebu. Na—naye Ireneo alilipinga kwa dhati, alilikanusha kabisa. Halafu basi, kama sote tujuavyo, ile hoja kuu ilikuwa ikija kwenye lile Baraza la Nikea; moja ya hoja kuu ilikuwa ni kama Mungu alikuwa *watatu* ama Mungu alikuwa *mmoja*. Naye Ireneo akachukua msimamo ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu, sasa, Mmoja tu.

<sup>9</sup> Huenda nikasoma kutoka kwenye *Wazee Waliotangulia Nikea*, juzuuy ya kwanza, ukurasa wa 412, nukuu ndogo tu; kama mnataka kuliandika, juzuuy ya kwanza ya *Wazee Waliotangulia Nikea*. Na katika ukurasa wa kumi na mbili, na ni ninii... Kama ultaka hiyo juzuuy, ni sehemu ya mwisho ya juzuuy ya tatu. Ungeweza kusoma hayo yote; kuna milango yake

kadhaa, ama sentensi kadhaa. Sasa ninaanza kusoma moja kwa moja mwishoni—moja kwa moja kwenye vifungu vyake ishirini, thelathini yya mwisho. Sitayasoma yote, bali sehemu yake tu:

“Matamshi mengine yote vivyo hivyo yakiwa . . . yanaleta sifa za Mtu yule yule mmoja,” (Mnaona, ye ye anajaribu kusema kile walichomwita Yeye, ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,’ naye alisema, “Hizo ni *sifa*, sio majina, sifa za huyo Mtu Mmoja.” Hicho ndicho hasa tunachofundisha hata wa leo.) “kama, kwa mfano” (na halafu katika mabano) “(katika Kiingereza), *Mungu mwenye Nguvu, Mungu Baba wa wote, Mungu Mwenyezi, Aliye Juu Sana, Muumba, Muumbaji*, na kadhalika namna hiyo. Haya si majina na sifa za mlolongo wa watu mbalimbali, bali wa mtu yule yule mmoja,” (Amina!) “kwa jina ambalo Mungu huyo mmoja, Baba, ni . . . Yeye—Yeye ambaye mambo haya yote . . . ridhaa ya ninii yote . . . ya maisha, fadhila ya uhai wote.”

<sup>10</sup> Ireneo anasema ya kwamba “Sifa hizi zote zinajumuishwa katika Jina moja, chini ya Mungu mmoja, nazo ni sifa tu za kile alichokuwa.” Yeye alikuwa Ua la Uwandani. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Hiyo ni sifa. Alikuwa Nyota ya Asubuhi. Alikuwa Alfa. Alikuwa Omega. Hizo ni sifa za kile alichokuwa. Alikuwa Baba. Alikuwa Mwana. Alikuwa Roho Mtakatifu. Bali kuna Mungu *mmoja*. Mungu mmoja, na Jina Lake ni Moja. Na hiyo ndiyo sababu moja nilifikiria Ireneo alikuwa sahihi katika—katika ubainishaji wake hapa, ama tafsiri ya Maandiko.

<sup>11</sup> Jambo lingine ambalo ningetaka kuwasomea, linapatikana katika kitabu *kiitwacho*: *Ilitukiaje?* Hiki kimeandikwa na wanahistoria. Na, *Ilitukiaje?* kilichoandikwa na R. C. Hazeltine, historia ya makanisa ya mwanzoni. Na hapa kwenye ukurasa wa 180: “Karama Za Kiroho Katika Wakati Wa Ireneo, mwaka wa 177 A.D. hadi 202.” Sasa, sababu ya mimi kunukuu haya, yanaingia kwenye kanda, mnaona, na—na yatatolewa kwenye vitabu:

“Ilikuwa ni katika wakati wa Ireneo ambapo karibu makanisa yote ya kimitume ya Ufaransa yalikuwa na karama za Roho Mtakatifu.” Hiyo ilikuwa ni kutokana na mafundisho yake, mnaona. “Washiriki wa kanisa la Ireneo huko Lyon,” hiyo ni Lyon, Ufaransa, “walinena kwa lugha. Halikuwa ni jambo lisilo la kawaida kumwona mtu aliyekufa akifufuliwa tena. Uponyaji ulikuwa—uponyaji ulikuwa jambo lililotukia kila siku katika ninii yote ya kiinjilisti . . . makanisa yote ya kiinjilisti kila mahali.” Ireneo huyo alijua jinsi ya kufundisha! “Miujiza ilikuwa ni jambo la kawaida. Kusema kweli, makanisa hayo hayakukosa madhihirisho ya kimiujiza ya uwepo wa Mungu labda kwa ono, kukomesha kwa maumbile, katika mwujiza, kuwakumbusha Wakristo wa kiinjilisti wa siku hizo, walikuwa wanafunzi Wake wapendwa. Lakini kutokana na historia za kale, hatuwezi kupata angalau mfano wa kuwafufua wafu katika kanisa la kwanza la Rumi.”

<sup>12</sup> Hao ni watu ambao hawaninii...hawapendelei upande wowote, wanasema tu ukweli. Ni wanahistoria.

<sup>13</sup> Hiyo ndiyo sababu ninawazia Ireneo, kwa sababu, mnaona, alikuwa na imani ile ile ambayo Paulo na wale wanafunzi waliirithisha. Hiyo ndiyo sababu nina...ninaamini ya kwamba alikuwa malaika wa kanisa la Smirna, kwa sababu alikuwa... alikuwa na mafundisho yale yale ya Kimaandiko; na mafundisho yale yale ya Kimaandiko juu ya msingi wa Neno la Mungu yatazaa kitu kile kile kila wakati. Kama utachukua tu fomula ya Mungu na kuitekeleza kikamilifu, haidhuru makanisa yanasesma nini, ulifuate jinsi tu limesema, litazaan kitu kile kile. Na hivyo ndivyo Ireneo alivyofanya.

<sup>14</sup> Sasa, nafikiri ya kwamba Polycarp alikuwa ni mtu mzuri, nafahamu; ila ninasema kwamba aliegemea kupita kiasi kwenye kuliundia kanisa dhehebu, na kama vile Wanikolai walivyokuwa wakifanya. Walikuwa wakiliundia kanisa dhehebu, na—na kuleta udugu pamoja. Ambalo linaonekana ni zuri kiakili, lakini, unaona, Roho yuko mbali sana na mambo ya kiakili hata...huwezi hata kuwazia vizuri kwa—kwa Roho. “Mawazo Yangu yako juu sana kuliko mawazo yenu,” asema Mungu. “Njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu.” Kwa hiyo kuna njia moja tu ya kufanya jambo hilo; mfuate tu kwa ramani iliyowekwa. Hiyo ni kweli.

<sup>15</sup> Sasa, huenda tukawazia, kama ulikuwa ukienda kutoka hapa...Kama nilikuwa nikienda Chicago usiku wa leo, huenda nikatoka hapa nje na kuchukua dira, na kusema, “Sasa, hebu tuone, Chicago iko moja kwa moja upande huu. Vema, nitaondoka mara moja.” Nisingeweza kutoka nje ya Jeffersonville. Mnaona? Sina budi kujitafutia ramani ya barabara. Na kuna—kuna ninii...kuna njia imewekwa ambapo ninaweza kwenda Chicago katika saa sita ama saba za usafiri wa gari, bali siwezi kukatia vyovyote. Ndege haiwezi kamwe kukatia vyovyote; ana m—mstari wa hewani ama urefu fulani na kadhalika anaopaswa kurukia, nyuzi fulani anazopaswa kukaa.

<sup>16</sup> Kuna njia iliyoandaliwa, na Mungu anayo njia. Mungu ana njia kwa ajili ya Kanisa Lake, kwa ajili ya watu Wake. Wala kamwe hakukusudia litawaliwe na mapapa, makadinali, askofu mkuu, ama waangalizi wakuu. Roho Mtakatifu ndiye mwalmi wa Kanisa la Mungu aliye hai, kuliendezea. Na utakatifu wote haumwendei kadinali ama kasisi, kumfanya mtu mtakatifu ka—kanisani, chochote kile. Walei wana haki tu...haki kwa Roho Mtakatifu kama mhubiri yeoyote, mchungaji, shemasi, mdhamini, yeoyote yule. Walei!

<sup>17</sup> Na sababu ya kuliita Nikolai...Kama tulivyosema jana usiku, Nikolai, tulilichambua neno hilo na kulitoa kwenye Kiyunani. Nalo N-i-k-o, lilimaanisha...*Niko*, ambalo maana

yake ni “kushinda ama kupindua.” Ati nini? N-i-k-o, Nikolai, *walei*. “Kuwashinda walei,” na kuwapindua kwa kuwapa utaratibu wa wanadamu, makasisi ambao ungewafundisha na ungeninii . . . wangefikia maamuzi yao wenyewe pamoja. Hivyo ndivyo lile Baraza la Nikea lilivyofanywa. Kwa sababu wengi walikusanyika na kutengeneza utaratibu katika Baraza la Nikea. Hatuninii . . . sitaki kuzungumza sana juu yake, maana hiyo ni ya Alhamisi usiku, katika Baraza la Nikea.

<sup>18</sup> Lakini hapo ndipo Kanisa Katoliki la Kirumi lilipoundiwa, kutokana na kundi la watu waliokuwa ni waongofu wa Mtakatifu Paulo, na Ireneo, na Mtakatifu Martin, na kuendelea. Walikuwa Wakristo walioongoka kwa . . . kutoka kwa upagani wakaingia Ukristo, bali walitaka kulirudisha kanisa nyuma kwenye mfano wa huduma ya Agano la Kale, kama vile kuwa na makuhani wakuu, na—na uhalifa wa kimitume, kama kutoka kwenye papa mmoja hadi papa mwagine, papa mwagine. Kama tungeendelea moja kwa moja kupitia katika Biblia hii, ungeona ya kwamba hiyo ni kweli kabisa na jinsi ambavyo Mungu alilihukumu jambo hilo tangu mwanzo kabisa; na wakati wa kanisa wa jana usiku, alisema, “Naichukia!” na vivyo hivyo na Kanisa.

<sup>19</sup> Mungu kamwe hakukusudia Kanisa liongozwe na wanadamu. Mungu huliongoza Kanisa Lake, Naye huliongoza kwa karama za Roho. Karama za Roho zimo kanisani kuisahihisha roho. Yeye ana ofisi tano za kihuduma Kanisani Mwake. Ya kwanza ni mitume, ama, wamishenari. Umishenari ndio wito wa juu sana uliopo, mtume. Neno *mmishenari* linamaanisha “aliyetumwa”; *mtume* linamaanisha “aliyetumwa.” Sababu ya wao kuchagua kuitwa mmishenari, sijui mimi. Lakini hao ni mitume. Vema. Mitume, manabii, walimu, wainjilisti, wachungaji. Sasa, hizo ni ofisi za Mungu zilizoteuliwa kwa Kanisa Lake.

<sup>20</sup> Halafu katika kila kanisa la mahali hapo mna karama tisa za kiroho zinazokuja mionganii mwa watu, hiyo ni kusema, maarifa, hekima, karama ya uponyaji, kufanya miujiza, kunena kwa lugha, kufasiri lugha. Na vitu hivi vyote vinaenda kwenye kila kanisa la mahali hapo. Na kila mtu kanisani ana huduma ya kibinagsi, na hiyo huduma ya kibinagsi inaabatana na huduma hizo zingine, kujenga Mwili wa Yesu Kristo. Wala kamwe . . .

<sup>21</sup> Sasa, kumbukeni jambo hili, ya kwamba hapa kuna . . . Nitaichora mistari hii usiku wa leo. Kanisa la kwanza, Efeso; Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, Laodikia. Sasa, kumbukeni wakati hii ikiendelea, kanisa *hili* liliwu na utimilifu wa Roho, bali mwishoni mwa wakati wa kanisa tunaona ya kwamba alikuwa akisukumiwa nje. Wakati wa kanisa uliofuata ukasukuma zaidi kidogo; zaidi kidogo; mpaka *huu*, kulikuwako na kipande kidogo sana. “Una mambo

machache,” Yeye alisema. Loo, tutakapoufikia Wakati huo wa Kanisa la Thiatira!

<sup>22</sup> Sasa, baada ya huyo kuja, Mungu alimwinua Mjerumani jina lake Martin Luther ambaye alilirudisha Kanisa tena. Lilianza kidogo zaidi, yeye alihubiri Kuhesabiwa haki; ndipo akaja Martin Luther, akahubiri Kuhesabiwa haki. Kisha akaja John Wesley na kuhubiri Utakaso. Ndipo katika wakati huu wa kanisa *hapa*, walirudi moja kwa moja tena kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu tena, pamoja na ishara zile zile na maajabu, zikishuka moja kwa moja. *Hapa* ndipo lilipotoka likapitia kwenye miaka elfu moja mia tano ya Nyakati za Giza. Na hapo ndipo ninii yenye giza sana...ama kipindi kirefu sana cha kanisa tulichokuwa nacho katika nyakati za kanisa. Halafu *hapa* ndipo linaanza kuinuka, Kuhesabiwa haki, Kutakaswa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nayu Biblia ilisema kwamba, “Mwishoni mwa wakati *huu*, ya kwamba hawa walio wachache watabanwa sana kwa sababu kanisa lile lile la Pentekoste litaanza kufanya jambo lile lile waliloanza *hapa* nyuma, Unikolai.” (Ee Mungu, hebu nifunge kinywa changu mpaka nitakapofikia hilo.) Mnaona? Kile ninachoweza kuona pale. Mnaona, mpaka mnapoweza kuona hapa. Nami nitawaonyesha ya kwamba mjambe wa wakati huu wa kanisa atayachukia madhehebu. Roho atainuka ndani ya watoto. Imekuwa hivyo daima. Na sasa tuna ninii...

<sup>23</sup> Sasa, kama utaangalia hili, jinsi liliwyokuwa kuu *hapa*, likatoka, na hatimaye likamtoa nje kabisa. Ndipo linaanza kurudi. Luther akalivuta nyuma, Kuhesabiwa haki; Utakaso; Ubatizo wa Roho Mtakatifu; halafu basi moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho kabisa, analisonga kabisa, mpaka Huyu karibu ametoka kabisa, kuna kiasi kidogo tu mle, na hapo ndipo yeye alipopiga makelele, “Kama hataifupisha kazi kwa ajili ya Wateule, hakuna mtu atakayeokolewa.” Mnaona? Haya basi, moja kwa moja katika wakati wa mwisho. Sasa kumbukeni hilo.

<sup>24</sup> Sasa tutaanza kwenye Wakati huu wa Kanisa la Smirna. Kwanza ninataka kuuchambua hapa kwenye karatasi fulani ni—niliyo nayo mimi. Sasa, wakati wa pili wa kanisa ukiwa ni Smirna, nami ninaamini nyote mtakubaliana nami (ama natumaini mnakubaliana nami, ama nusu, haidhuru) kwamba Ireneo alikuwa ndiye nyota ya wakati huo wa kanisa. Yeye alikuwa mjambe wa Mungu kwa sababu aliizunguka nchi hiyo, akaingia Ufaransa (Gaul), huko chini, naye akaanzisha makanisa, na kila moja ya hayo lilianzishwa juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, kuwafufua wafu, kuwaponya wagonjwa, kuikomesha mvua, na kufanya miujiza kila siku. Walijua ya kwamba Mungu aliye hai aliishi mionganoni mwa hao watu. Huyo alikuwa ni mtu wa Mungu, maana Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kufanya...” Ama wa-watu walisema, “Hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya

isipokuwa Mungu yu pamoja naye.” Ilikuwa ni Nikodemo aliywambia Yesu hivyo.

<sup>25</sup> Sasa, mji wa biashara; kituo cha biashara kilichoelekezwa kwa Lydia na magharibi. Mji wa tatu kwa ukubwa katika Asia, jiji kubwa la bandarini. Ulisifika kwa utajiri, mahekalu, mijengo, shule, tiba na sayansi. Wayahudi waliishi S—Smirna, nao wakawahubiria injili watu wa Smirna. Polycarp alikuwa ndiye askofu wa kwanza wa Smirna. Polycarp na watumishi wengine waaminifu waliwekeea msingi imani yenyе kilindi ya Mungu kwa Wasmirna walioamini. Wazee wa mwanzoni wa kanisa waliipa Smirna ushawishi wa Kweli.

<sup>26</sup> Wakati wa kanisa la Smirna, jina la kanisa hilo lilikuwa Smirna, *Smirna*, hasa, hilo linamaanisha “uchungu,” manemane. Linahusishwa na mauti, maana walikuwa wanakufa.

<sup>27</sup> Kanisa lililotesa, Mungu aliwaita “walioteswa.” Mungu aliangalia mateso yao, na kuwapa neema ya kuyavumilia. Aliangalia dhiki yake, na kuwapa ushindi juu ya mauti. Aliangalia umaskini wao, akawapa utajiri ndani Yake. Kanisa la Smirna lilipitia tanuru ya dhiki iliyowaka moto ya dhiki, bali, lilikuwa harufu nzuri Kwake. Hiyo ni hao Masalia sasa, sio kanisa zima la Smirna; Masalia tu ndio ninaonena habari zao. Zile *siku kumi za dhiki* zinamaanisha “miaka kumi ya mateso yenyе umwagikaji mkubwa mno wa damu.”

<sup>28</sup> Sijui kama ninaweza kuendeleza herufi za jina hili, ama kulitamka, ama siwezi. Huyu alikuwa ni mfalme mkuu wakati huo, ninaamini alikuwa aliywaga damu sana kuliko wote tangu Nero katika mwaka wa 67, D-i-o-c-l-e-t-i-a-n. Kwenye mwaka wa 303 hadi 312 A.D.

<sup>29</sup> Mungu anawasihi Smirna wawe waaminifu hata kufa, kama Yeye alivyokuwa, “Nami nitawapa taji ya Uzima, kama vile Baba alivyonipa Mimi.” Mungu alimwahidi mshindi (katika dhiki) ushindi juu ya mauti ya pili, “Msiogope hao wanaoweza kuua mwili, bali Yeye anayeweza kuiangamiza nafsi, ama kuiua nafsi.” Hiyo... Wasmirna walipaswa wavumilie hata mwisho, “Msiwaogope wanadamu, na taji ya Uzima mtapewa.” Mateso ya Ukristo katika zile nyakati yameainishwa katika nyakati za kanisa, wa Smirna, ni muhimu sana. Tutapenda kuuendea katika muda mfupi tu, Bwana akipenda.

<sup>30</sup> Sasa, kama baadhi yenu mkikosa baadhi ya haya wakati... kama nikiyaandika upesi kupita kiasi kwa hao wengine darasani, basi tutaninii...tumaninii...hakika mnawenza kuyapata kutoka kwetu wakati wowote mtakao, tutafurahia ku—kuwapa. (Samahani.)

<sup>31</sup> Sasa katika mlango wa pili na kifungu cha 8, tunaanza usiku wa leo. Sasa, tulimwacha wapi jana usiku? Hakika alikuwa... aliuchukia huo Unikolai. Hiyo ni kweli? Sasa Mungu anafanya nini? Tunapaswa kuwa tumeona nini kwanza? Ufunuo wa Yesu

Kristo, kwamba Yeye ni Nani na kile Yeye alichó. Sasa jambo lingine kuu, tunaona ya kwamba anachukia kitu chochote kitakachoweka kitu chochote kulitawala Kanisa Lake mbali na Yeye Mwenyewe. Yeye ni Mungu mwenye vivu.

<sup>32</sup> Jinsi ningetaka kusimama, maana tuna vifungu vinne tu hapa, kunukuu tu kitu kidogo. Ni wangapi wanaweza kukumbuka wakati yule nabii mwema, Samweli, wakati Israeli wote walipotaka kufanya kama walimwengu wengine? Mnakumbuka hilo? Naye nabii akawaambia, kasema, "Mmekosea!" Lakini walitaka kufanya kama Wafilisti, na kama ha—hao wengine. Vema, hilo ndilo lilitotukia hasa katika wakati huu wa kwanza wa kanisa. Ni ajabu kwamba watu hawataki Mungu awaongoze. Wanataka kufuata... wanataka mitu fulani. Israeli, ilifanya kosa mbaya kuliko yote iliyowahi kufanya, wakati... Neema ilikuwa tayari imewapa nabii, kiongozi, ikawapa mwana-kondoo wa upatanisho, na kuwapa chakula kutoka mbinguni, na mambo yote mazuri ambayo neema ilikuwa imewapa, na bado, katika Kutoka 19, walitaka sheria. Walitaka kuwafanya madaktari wa uungu, na kuwapata watu, walitaka kuwa na kitu fulani cha kufanya katika Hilo, pia.

<sup>33</sup> Mwanadamu sikuzote anajaribu kumshinda akili Muumba wake aliyemuumba, wala hafanyi kitu ila kujiua mwenyewe. Kama vile Jumapili chache zilizopita nilihubiri juu ya Di—Dini Chotara. Na hiyo ni hakika. Unapochanganyishia mbegu kitu chochote, kamwe hakiwezi... kimekwisha! Kimeisha, hakiwezi kurudi tena. Nyumbu hawesi kuzaa tena na kupata nyumbu mwingine, kwa sababu yeye—ni nyumbu, ni chotara. Mhindi mzuri, huwezi kukuza mahindi mazuri kutokana na mahindi chotara. Hata hayataninii... Huenda yakachomoza, bali ni—ni, loo, hayafai kitu hata kidogo. Huwezi kuyakuza. Kitu chochote chotara hakifai kitu.

<sup>34</sup> Nayo dini chotara haifai kitu! Almuradi unajaribu kuongeza kitu fulani kwa yale Mungu alisema, ama kufanya jambo ambalo Mungu hataki ufanye, ni dini chotara. Huenda yakaonekana ya kupendeza. Loo, mahindi chotara yatang'aa kuliko mahindi asilia. Na maskini nyumbu atawashinda kazi farasi wawili. Vema, hiyo ni... Haifanyi kazi, ndugu, tunaokolewa kwa neema. "Hatuokolewi kwa matendo, bali kwa neema." Kwa hiyo huenda hiyo... Natumaini hamtafikiri matamshi haya... Mme—mmeketi chini ya hangaiko, nami na—naihisi hapa juu. Mnaona? Kwa maana kuna Wapresbiteri, Wamethodisti, na wa kila namna hapa ndani. Tunajua hilo. Na kwa hiyo ni—ninaihisi. Nanyi inawapasa kustarehe kidogo mara kwa mara, muutikise huo, kwa namna fulani.

<sup>35</sup> Sasa, sikilizeni. Chochote chotara hakifai kitu. Inakupasa kuchukua cha asili, jinsi Mungu alivyokiumba, ndipo una kitu ambacho ni halisi.

<sup>36</sup> Sasa, tunaona ya kwamba basi kanisa hili la Israeli, wakati wakipita, Mungu alikuwa amewalisha, na kuwashughulikia, na kuwafanyia kila kitu. Basi hatimaye wakaangalia kwa Wafilisti, na Waamori, na . . . na wengine mbalimbali, na kusema, “Tunataka mfalme! Wana kitu tusicho nacho.”

<sup>37</sup> Hilo ndilo jambo lile lile watu wafanyalo leo hii. Mmoja wa hawa, dada zetu, ataangalia kwenye televisheni na kumwona Gloria Swanson, ama ye yote wao. . . baadhi ya hao wanawake waliovaa nguo ya aina fulani, nao hawawezi kuvumilia mpaka wapate moja. Mnaona? Mnawaona wanawake katikati ya mji, “Loo, hiyo si ni nzuri sana?” Unajali nini kile angevaa? Watu, wako hivyo tu, nilisema ni siku ya u—uigaji, mtu fulani anataka kuiga huyo mwingine. Hebu chukua. . . Kuna Elvis Presley wengi sana sasa, na—nawaambieni, usingeweza kuwalundika kwenye mabehewa, kwa sababu amekuwa maarufu katika ninii ya kimwili. . . uigaji!

<sup>38</sup> Tuna jambo lile lile katika dini. Ninii. . . Nilikuwa nikisoma historia ya Martin Luther, na ye yote wenu wanahistoria mnajua. Walisema haikuwa ni jambo la ajabu kwamba Luther angeweza kulipinga kanisa Katoliki na kupita nalo, bali ajabu kubwa zaidi, ni kwamba angeweza kushikilia kichwa chake juu ya ulokole wote uliofuatana na uamsho wake na bado adumu na Neno. Huo ndio mwujiza, jinsi ambavyo Mungu alimweka huru na mnyofu.

<sup>39</sup> Sasa, kwa hiyo wakamjia huyu Samweli. Wakasema, “Tufanyie nab. . . ama tufanyie m—mfalme.” Naye Bwana akamwambia ya kwamba alilikataa wazo hilo, jinsi hasa alivyolikataa hapa kwa madhehebu.

<sup>40</sup> Kama tu vile alivyolikataa hilo, Yeye anayakataa madhehebu. Hakatai utaratibu, bali dhehebu. Mpangilio, hatuna budi kuwa nao. Lakini dhehebu haitubidi kuwa nalo, kwa maana huchora mipaka: “Sisi ni *Fulani-fulani*.” Je, wewe ni Mkristo? “Mimi ni Mmethodisti.” Je, wewe ni Mkristo? “Mimi ni Mbaptisti.” Hilo halimaanishi zaidi ya nguruwe katika zizi. Hilo halina uhusiano wowote Nalo, hata kidogo. Mkristo!

<sup>41</sup> Nilimwuliza msichana mmoja usiku mmoja, jukwaani, “Je, wewe ni Mkristo?”

Akasema, “Mbona, nataka uelewe, ninawasha mshumaa kila usiku.” Kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote na Ukristo!

<sup>42</sup> Mwanamume mwingine akasema, “Vema, mimi ni Mmarekani. Hakika!” Vema, hilo halina uhusiano wowote Nalo, hata. Wewe ni Mkristo kwa sababu wewe ni mwenyeji wa Ufalme mwingine. Hiyo ni kweli. Nawe uko—uko katika Ufalme mwingine, wa huko juu.

<sup>43</sup> Sasa, Samweli alifanya nini? Jambo lile lile tu ambalo Mungu alifanya hapa. Samweli aliwaita Israeli pamoja, akasema, "Sasa, nisikilizeni. Ninataka kuwaaulizeni jambo fulani. Pamewahi kuwapo na wakati ambapo nimepata kuwaambia jambo lolote ambalo halikuwa ni kweli?" Kasema, "Mi—mimi ni nabii wa Mungu mionganoni mwenu. Niambieni wakati mmoja niliopata kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia." Hivyo ndivyo Samweli alivyowaambia. Alisema, "Na hivi Mungu hajawalisha na kuwashughulikia na kufanya mambo haya yote?" Kasema, "Mnatenda dhambi kwa kujaribu kufanya kama mataifa mengine."

"Loo . . ." wakasema.

<sup>44</sup> Akasema, "Nataka kuwaauliza jambo lingine. Nimewahi kuchukua pesa zozote kutoka kwenu? Nimewahi kuwaomba sadaka? Ama je, nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia?"

Wakasema, "La. Kamwe hukuchukua pesa zetu, hiyo ni kweli. Wala hujawahi kutwambia lolote katika Jina la Bwana ambalo halikutimia."

Akasema, "Basi nisikilizeni! Mnatenda dhambi kwa kujaribu kufanya kama hao wengine." Lakini walitaka mfalme kwa vyovoyote vile! Haidhuru kama ilikuwa ni sawa ama si sawa, wa—walitaka kulitekeleza wazo lao.

<sup>45</sup> Hilo ni jambo lile lile kanisa lililofanya papa hapa katika Efeso, walichukua fundisho la Nikolai. Na walipolichukua, liliwasukuma moja kwa moja kuunganisha upagani na Ukristo pamoja na kusababisha miaka elfu moja mia tano ya Nyakati za Giza. Ndipo wakati Luther alipowavuta nje, kama (zamu ya pili) Walutheri hawakufanya jambo lile lile walilofanya huko Efeso! Kweli kabisa.

<sup>46</sup> Sasa, kama utaangalia, vinara vya taa havikukaa *hivyo* hasa. Vilianza chini *hivi* vikaja juu. Vema, kile kirefu zaidi mbali na mahali alipokuwa amesimama kilikuwa hiki *hapa* juu. Ndipo Ukristo polepole ukasongwa kabisa wakati ukitoka mahali Yeye alipokuwa amesimama katika umbo la msalaba, kama vile tungemwona Yeye katika mlango wa 4; katika umbo la msalaba namna *hii*. Nao *huu* ni mkono Wake wa kulia, *ule* ulikuwa ni mkono Wake wa kushoto. Sasa, papa *hapa*, Yeye alikuwa ameweka mkono Wake juu ya kanisa *hili* na juu ya kanisa *lile*. Alikuwa ni Alfa na Omega pia na, hakika, zote zilikuwa katikati ya haya mawili, nyaraka zingine zote. Lakini Yeye hasa alisema, "Alfa na Omega." Yeye alikuwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, ambao ulikuwa ni agano Lake.

<sup>47</sup> Sasa, kama ukiangalia, nuru ya Pentekoste, mahali ilipoanza, polepole ilizima. Hawa watu, Ireneo, Polycarp, na hao wengine wote walitia muhuri ushuhuda wao kwa damu

yao, mpaka hatimaye ikausukuma Ukristo ukaingia katika siku zenygiza kuliko zote.

<sup>48</sup> Sasa angalieni, ule wakati wa kwanza ng'ambo ya lile nundu kuu, ikija ilikuwa ni Nuru ndogo, Nuru zaidi, kisha Nuru zaidi. Angalia jinsi inavyoanza kumulika tena, kufikia siku ile. Na sasa mwishoni mwa wakati *huu*, imebashiriwa hapa kwamba litafikia kwenye *Laodikia*, "vuguvugu." Sasa, hili hapa. Mbona, kama kitu *hiki* hapa kiliwaleta kwenye *hiki*, kwa nini tupende hicho hapa chini katika Pentekoste?

<sup>49</sup> Nanyi mnajua ya kwamba Biblia ilisema, "Atatokea mnyama." Nasi tunajua huo ni upapa wa Kirumi. Hiyo ni kweli kabisa. Ndipo wangefanya sanamu ya huyo mnyama. Sanamu ni nini? Kitu kilichofanywa kama huyo. Na hiyo ni muungano wa makanisa, na Pentekoste iko ndani yake. Utakuja wakati ambapo ama utakuwa mfuasi wa dhehebu fulani au huwezi kuufungua mlango wako. Sasa mtaona kama hilo si kweli! Hiyo ndiyo sababu tunayashambulia hata kufa. Naam, bwana. Huwezi... Chini kuliko hayo, watajaribu kuwadunga sana, hata watajaribu kuninii... hawatakuruhusu kununua wala kuza isipokuwa uwe na alama hiyo ya madhehebu juu yako. Inaingiza moja kwa moja ndani.

<sup>50</sup> Ni kama tu siku ile hasa, waliwachoma moto, walininii... Nilisimama pale kwenye uwanja huo wa michezo; nikalia kama mtoto mchanga nilipoangalia kule juu ambako wapiganaji wangeketi kwenye maskini ule uwanja wa kale pale. Na-na kuviona vitu hivyo, na kujuu ya kwamba wengi wa ndugu zangu Wakristo waliliwa na simba na-na kuraruliwa vipande-vipande mahali pale, na wanawake na watoto wadogo na kadhalika. Nami nafikiri, kama wote walikufa katika imani, ningewaaibisha sasa? La, bwana, ndugu! Mungu, nijalie niitetee Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja! Jambo lile lile, hata liwe lisilopendwa na watu jinsi gani...

<sup>51</sup> Mtu fulani daima anataka kusema, "Vema..." Mtu fulani alisema si muda mrefu uliopita... Loo! Ni wahudumu wangapi mashuhuri hudumani wamenipigia simu na kusema, "Ndugu Branham, usipoachana na jambo hilo, kila dhehebu litakuchukia."

<sup>52</sup> "Mbona," nikasema, "kuna Mmoja ambaye hatanichukia, huyo ni Yule aliye Mbinguni. Huyo Ndiye ninayemtafuta." Mnaona? Sasa, mimi nawapenda watu katika kila dhehebu. Hakika. Lakini nimepata kuwaambia lolote ambalo Bwana... katika Jina la Bwana, halikutimia? Mnaona? Kila kitu kimesemwa na kutendwa vizuri? Nimewahi kuwaomba fedha? Basi kaeni mbali na madhehebu! Ninyi iweni huru katika Kristo, acheni Roho Mtakatifu daima aingie na kutoka kanisani.

<sup>53</sup> Jambo pekee ni kwamba, ondoleeni mbali tofauti hizi ndogondogo kutoka kwenu. Itikadi ndogondogo, na hisia

ndogondogo za ajabu-ajabu kwa ndugu zenu, na vitu kama hivyo, zitikiseni ziondoke! Msiache shina lolote la uchungu kamwe lichipuke nafsini mwenu. Mkiliruhusu, litawaozesha. Kweli. Dumisheni upendo! Sijali watu wanawachukia kiasi gani, wapendeni kwa vyovyote vile. Ikiwa hamwezi kufanya hivyo, mnahitaji... ninii... nyinyi hamjaninii... hamjatiwa muhuri, mna mahali palipolegea bado. Kwa hiyo njoni, rudini, mkatiwe muhuri vizuri sana kwa Damu ya Kristo. Itawasafisha na shina lote la uchungu. Naam.

<sup>54</sup> Sasa, mnaona, lakini tunajaribu tena. Baraka za Kipentekoste zilishuka yapata mwaka wa 1906, mahali fulani mle ndani. Yupo mhudumu anayeketi pamoja nasi usiku wa leo, mmishenari kutoka Tibet, mmoja wa walio wa... sisemi hilo kwa sababu yupo; natumaini hakwenda nyumbani. Nafikiri angali hapa, alikuwa atuhubirie kidogo kabla siashuka kuja. Na huyo mtu anakumbuka Pentekoste ya kwanza. Hapakuwepo na dhehebu lolote, kila mtu alikuwa na vitu shirika. Loo, jinsi iliyvo rahisi kupiga hatua mbaya papo hapo, na jinsi linavyoonekana ni jambo zuri kwa wenyewe elimu.

<sup>55</sup> Angalieni, Israeli hawakujua kabisa wakati walipokuwa wamesimama pale ukingoni, wakipiga makelele... Sasa, unasema, "Aina hii ya dini ni kitu kipyा." Mbona, ndiyo ya kale sana iliyopo. Hakika. Hata kabla ulimwengu haujaumbwa, walikuwa wakipiga makelele na kumsifu Mungu. Mungu alisema hivyo, alimwuliza Ayubu, "Alikuwa wapi hapo ninii—hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu wakapiga makelele kwa furaha." Hiyo ni kabla ulimwengu haujapata kuumbwa.

<sup>56</sup> Lakini sasa waangalie Israeli, walikuwa wameona miujiza. Hao ni wale Wapentekoste wa mwanzoni; Israeli, Pentekoste ya siku hiyo. Sasa walikuwa wametolewa Misri, Mungu alikuwa amewabariki, akawapa kila namna ya ishara kuu na maajabu, na kuwakomboa. Ndipo waliposimama hapo ukingoni na kufanya mkutano wa Kipentekoste... Waliufanya! Sasa sikilizeni. Musa alimba katika Roho, naye Miriamu akachukua tari na kukimbia ukingoni, akipiga tari hii, akicheza katika Roho; nao binti wa Israeli wakamfuata, wakicheza katika Roho. Kama huo si mkutano wa Kipentekoste, sijawahi kuona mmoja. Hawakuamini kabisa ya kwamba n—nchi ya ahadi ilikuwa miaka arobaini mbele yao. Ilikuwa yapata maili arobaini tu. Lakini ingewachukua miaka arobaini kusafiri maili arobaini kwa kuwa walichagua kitu kibaya. Walichagua kuwa na sheria badala ya kumwacha Roho Mtakatifu awaongoze, ile Nguzo ya Moto iwapeleke na kuwaongoza. Walitaka kuwa na jambo la kufanya wao wenyewe; walitaka kuwa na makuhani fulani, na watu fulani mashuhuri, na maskini theolojia ambayo wangegombania, badala ya kuendelea tu na kumruhusu Roho Mtakatifu awaongoze. Walikuwa katika Roho; Mungu alikuwa

amewapa kila kitu, bali iliwabidi kuwa na jambo fulani la kufanya ndani Yake.

<sup>57</sup> Ni kama tu kuchanganya mbegu tena. Achaneni na ng'ombe. Achaneni na farasi. Achaneni na chakula. Wao... Sayansi ilidai, katika *Reader's Digest*, makala yake, kama wakiendelea kuchotarisha chakula, na watu wanakila... Kama vile kuku, wamemdhoofisha kuku huyo sana hata hana mabawa wala miguu. Na kama akitaga mayai, anataga hata akafa, wanawenza kuishi tu mwaka mmoja. Nazo tishu ni nyororo sana ni vigumu kumla. Nao watu wanaomla, anawapotosha watu. Hiyo ni kweli.

<sup>58</sup> Mwajua, ulawiti umeongezeka yapata asilimia arobaini Marekani, katika mwaka mmoja uliopita. Na je, mlilia ya kwamba sayansi inadai ya kwamba wanawake wanakuwa wapano mabegani mwao na wembamba nyongani, nao wanaume wanakuwa wembamba mabegani mwao na wapano nyongani? Mnakula mbegu zilizopotoshwa, mnakula vitu vilivyopotoshwa. Mwili wako uliumbwu upate kustawi kwa vitu vya asili. Nacho kinafanya nini? Hata kinabadilisha mtiririko asilia wa wanaume na wanawake, mpaka Hollywood, hata serikali yetu, na kila kitu kimejaa wapotovu. Anafanya nini? Wanajiletea hayo wenyewe kwa mti wao wenyewe wa maarifa, wanajiuwa wenyewe.

<sup>59</sup> Rudini hapo mwanzoni! Achaneni na maumbile. Achaneni na Mungu. Liwekeni Kanisa katika Roho Mtakatifu; na muwaondokee maaskofu hawa wote na mapapa wenye kila namna ya fundisho. Rudini mahali tulipoanza. Rudini. Yesu angalikuja usiku wa leo, ungesema, "Mimi ni Mmethodisti."

Angesema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo!"

"Mimi ni Mpresbiteri."

"Haikuwa hivyo tangu mwanzo!" Ni kitu gani kilichokuwako hapo mwanzo? Ujuzi wa Kipentekoste wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo ilivyoanza.

<sup>60</sup> Lakini, mnaona, ilibidi tulipotoshe. Loo, inalifanya la kupendeza zaidi. Hakika. Lile kanisa dogo kule chini likicheza, na kupiga makelele; na kushuka mtaani, na watu wakiwatupia mawe, wakiwadhihaki, na kila kitu namna hiyo. Hilo halipendezi sana. "Lakini sasa tunayo Doksolojia kuu, na Kanuni ya Imani ya Mitume, na, loo, Daktari Ph.D., L.L. L. maradufu D., *Fulani-wa-fulani* kama mchungaji wetu." Nao wanatoka na kusema, "Ah-mina," kama ndama mwenye magango, na kuendelea namna hiyo, mambo hayo yote ya namna hiyo.

<sup>61</sup> Samahani, si—sikumaanisha kusema hivyo. Samahani, sikumaanisha kusema hilo namna hiyo. Mnaona? Sikumaanisha hilo. Hilo halimpasi mtumishi wa Mungu.

<sup>62</sup> Lakini, angalieni, hayo yote, mimi... ndio kwanza liingie niani mwangu, mnaona. Lakini kusimama na kusema mambo

hayo yote mbalimbali namna hiyo, kujizoeza kabla...mwajua, kusema, "Sasa, la, hulisemi hilo vizuri. 'Ah-mina.'" Ninapenda mkutano mzuri wa kale wa kipentekoste, ambapo nguvu za Mungu zinashuka, nawe unapiga tu makelele na kupaza sauti na kumsifu Mungu, ukiwa na wakati mzuri sana. Hivyo ndivyo; Roho amewashika hao watu. Lakini sisi...Ni vigumu kusikia "Amina!" tena, ni "Ah-mina." Hata hivyo, hapo ndipo tunapofikia, mnaona. Madhehebu haya magumu, kiburi...

<sup>63</sup> Sasa je, mitu...Kulikuwa na unabii kuhusu hilo? Mnakumbuka unabii wa Paulo jana usiku? "Najua kwamba baada ya kuondoka kwangu, mbwa mwiti wakali wataingia mionganoni mwenu, na watu wa tabaka lenu wenyewe, nanii wenu...mumo humo kanisani mwenu (hao wa kanisa Katoliki la Kirumi, wakiinuka) watainuka mionganoni mwenu na kuwavuta wanafunzi wawaafuate." Nao mbwa mwitu wa Paulo, tunaona, walifanyika Wanikolai.

<sup>64</sup> Msikilizeni Roho akizungumza kupitia kwa nabii tena, "Katika siku za mwisho kutakuwako na nyakati za hatari, kwa kuwa watu watakuwa wenyewe kujipenda wenyewe, ("Mimi ni Daktari Nanii wa nanii, usiniambie vipi kulihsu, sasa. Nataka ufahamu kwamba mimi ni Mpresbiteri. Haleluya!' Ama, 'Mimi ni Mpentekoste.')." Hiyo inaleta tofauti gani, kama wewe si Mpentekoste kwa asili? Ule ujuzi wake, unaona. Naam, bwana. "Mimi ni mfuasi wa Assemblies." "Mimi ni mfuasi wa Church of God." Vema hilo...hiyo inaleta tofauti gani kwa Mungu? Inakupasa kuwa mshiriki wa Ufalme wa huko juu, unaona. Hiyo ni kweli.

<sup>65</sup> Sasa, kama—kama ukiiona, ninii...mambo hayo yote ni mkusanyiko wa—wa mipepesuko. Sasa, lilisema, "Wangekuwa wakaidi, wenyewe kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Loo, hawawezi kwenda kanisani Jumapili usiku mradi tu kuna kipindi kizuri cha televisheni kinachoendelea. Loo, jamani! Daima wao...Hata makanisa yana timu za mpira, na supu ya jioni, na karamu za mchezo wa kriketi, na, "wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiowapenda walio wema." *Hawa* wakiwadharau *wale*, mnaona. *Hawa* wakiwadharau *wale*, wakiwasonga. Wasiowapenda *walio* wema.

<sup>66</sup> Loo, unasema, "Hao ni Wakomunisti, ndugu." Loo, la. La, la.

<sup>67</sup> "Wakaidi, wenyewe kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda walio wema, wenyewe *mfano*..." Ujuzi wa kimadhehebu, mnaona. "Wakiwa na *mfano* wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake."

<sup>68</sup> Ungekuwa nini katika siku hii? Unaona, "Wenyewe *mfano* wa utauwa." Unaenda kanisani kwa uchaji tu uwenzavyo, Jumapili, kisha unavaaa kaptura Jumapili alasiri, unakata nyasi uani na

kuwaita Oertel 92. Naye mchungaji anatoka nje na kuvuta sigara na kurudi, mwajua. "Wenye mfano wa utauwa!"

<sup>69</sup> "Vema, mchungaji, wana kanisa kule juu, wananiambia ya kwamba mama mmoja aliponywa hivi majuzi kutokana na kan-..."

"Hmm. Hmm. Upuuzi! Siku za miujiza zimepita."

<sup>70</sup> "Vema, mnajua nini? Ni—ni—nilikuwa huko juu kwenye kanisa dogo hivi majuzi usiku, ile misheni ndogo huko chini pembedi, na kulikuwako na mtu fulani aliyejewa akienda pale juu, akisema kitu fulani, akip-..."

"Loo, kipenzi, kamwe usikikaribie kitu kama hicho. Hao ni mbwa wendawazimu. Jamani! Usiwakaribie hao. Hao ni watakatifu wanaojibingirisha. Kamwe usininii..."

<sup>71</sup> "Wenye mfano wa utauwa bali wakikana nguvu zake, hao nao ujiepushe nao. Kwa maana hawa ndio waendao nyumba hata nyumba na kuwashika mateka wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa nyangi, wasiweze kujifunza wala kuufikia ujuzi wa ile Kweli." Hiyo ni kweli kabisa. Haya basi, shirika la kina mama la msaada, shirika *hili, lile*. Maskini kanisa hilo lina mashirika mengi sana hata haliwezi kuihubiri Injili tena. Mchungaji hawezi kupata ila dakika ishirini, na inambidi kuzungumza juu ya jambo lingine basi. Mnaona? Wasipofanya hivyo, halmashauri ya mashemasi watakutana naye. Naam, bwana.

<sup>72</sup> Loo, ndugu, mchungaji mzuri inampasa kufanya nini siku hizi? Kufanya tu vizuri awezavyo kusimama na kupogoa matawi mahali wanakotaka, na kuacha vibanzi vianguke vitakapo; na kulivurumishia pale. Hivyo tu. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Usi—usimwachilie mtu yejote, lihubiri tu Neno na udumu moja kwa moja Nalo, lishindilie tu. Kama wakikutupa gerezani, lihubiri gerezani. Kama ukiwekwa mahali pengine popote, hubiri kila mahali uendapo; endelea tu kusonga mbele, ukihubiri. Hiyo ni kweli. Sasa, hilo ndilo limetukia. Mnaona, wanaizima.

<sup>73</sup> Sasa tunakuja kwenye—kwenye Wakati wa Smirna. Kifungu cha 8:

...kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika;  
Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa  
mwisho, aliyejewa amekufa, kisha akawa hai.

<sup>74</sup> Ninataka muone kila wakati anapoitambulisha Mwenyewe kwa wakati wa kanisa, Yeye anaweka kitu fulani cha Uungu Wake. Hicho ndicho kitu cha kwanza anachojaribu kulijulisha kanisa, hicho, hicho ni Uungu Wake. Yeye ni Mungu! Mnaona ile hoja kuu hapa nyuma ambayo Ireneo na hao wengine walikuwa wakibishania? Walijaribu kusema ya kwamba Mungu katika ulimwengu tatu, na ni Mungu katika watatu, na Mungu

katika *hili*. Akasema, “Hakuna kitu kama hicho! Ni sifa za Mtu mmoja, na huyo ni Mwenyezi Mungu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo huninii... daima wamekuwa na hilo. Naye Mungu hapa katika mwanzo anajitambulisha Mwenyeewe katika moja ya ninii Wake—wa Uungu Wake. Mnaona Yeye anajitambulisha Mwenyeewe, kwanza hapa, “Mimi Ndimi aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Nami ni Mwenyezi.” Hapa anaanza moja kwa moja na Wakati wa Smirna sasa.

<sup>75</sup> Sasa msikilizeni, “Mimi . . .”

. . . *kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna . . . (Nasi tunaamini kwamba huyo ni Ireneo.) . . . andika; Hayo ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa mwisho, . . .*

Mnaona? Akajitambulisha Mwenyeewe, “Mimi ni Mungu, sasa, wa wakati huu wa kanisa. Sitaki miungu wanne ama watano mbalimbali hapa. Mi—mimi ni Mungu. Mnaona, jambo ndilo hilo.”

. . . *aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai. (Amina!)*

<sup>76</sup> Sasa, huo ndio—ndio utambulisho. Sasa—sasa *Smirna* inamaanisha “uchungu,” na inatokana na neno manemane—manemane. Na kanisa la—la kwanza—kanisa la kwanza, na . . . lilikuwa limepoteza upendo wao wa kwanza, kanisa la Efeso. Nalo kanisa hili lilikuwa limeanza kuwa na “shina la uchungu” likichipuka ndani yao kwa kuwa kanisa hili, kanisa kuu, sehemu kubwa (walio wengi, sikuzote) walikuwa wakipinga sana Roho Mtakatifu kulitawala kanisa, nao walitaka kutawala, wenyewe. Walitaka kuweka ukasisi, walitaka kufanya kama watu wa Agano la Kale walivyofanya. Walitaka makassis. Nao . . . Kama miungu wa kipagani, huko nyuma, ambako waliongokea, walikuwa na makuhani na kadhalika wa . . . wa Jupita, na makuhani wa Venasi, na kadhalika; wa—wa—wanataka kuingiza kitu hicho hicho na kuwafanya watu *hawa*. Mnaona, chanzo cha kitu hicho chote ni upagani. Wapagani wote wana makuhani hao na vitu kama hivyo. Lakini—lakini Kanisa la Mungu aliye hai, ni geni kwao. Kristo ndiye Kuhani wetu, Kuhani wetu Mkuu. Tunaye Kuhani Mkuu, meza pia ambayo tunakulia.

<sup>77</sup> Sasa, kanisa hili lilikuwa limeanza kuchipusha “shina la uchungu.” Kwa nini? Liliona uchungu juu ya wale wanaotaka kuendelea na Roho Mtakatifu. Upendo ulikuwa umefifia, nao walikuwa wakijaribu kuubadilisha kwa kanuni za imani na madhehebu, wakiuacha uongozi wa Roho Mtakatifu. Wazia hilo! Hiyo ndiyo sababu u—u—uchungu ulikuwa ndani yao. Vema.

<sup>78</sup> Sasa, kanisa la kwanza, hili . . . uchungu uliana kunyemelea. Kanisa la pili, zaidi kidogo. Na, hatimaye, uliingia moja kwa moja ndani kwa sababu walikuwa wakiunda “kanisa bora zaidi”; walidhani hivyo. Papa hapa walikuwa na kitu cha kiungwana, wale watu mashuhuri wa Kirumi wangeweza kuingia mle. Kwa nini? Walikuwa na papa, walikuwa na—

walikuwa na watu mashuhuri, makadinali, na kadhalika. Walivalia nadhifu. Waliachana na kelele zote na kila kitu walichokuwa nacho; wakawa wanyamavu sana. Ilionyesha walikuwa wanakufa. Uh-huh. Uh-huh. Walikuwa wanakufa. Na kwa hiyo wakawa waheshimiwa na kuunda shirika bora zaidi. Jambo la kwanza hapa juu, waliweka kitu hicho chote katika dhehebu kubwa la kikasisi, kanisa la Ulimwenguni Mwote la Kirumi, kanisa Katoliki la Kirumi katika ule Wakati wa Giza. Vema, basi, walikuwa na waheshimiwa, na walikuwa na tabaka.

<sup>79</sup> Loo, lilikuwa ni la kupendeza zaidi kuliko wakati walipokuwa wakisimama mtaani, “na kuwabidi kutembea wamevikwa ngozi ya kondoo kama ngozi ya mbuzi, na wakiwa, na kukatwa kwa msumeno, na—na kuchekwa, na kudhihakiwa,” na kama vile Paulo alivyosema katika Waebrania mlango wa 11.

<sup>80</sup> Mbona, kanisa hili kubwa, mashuhuri, lenye majoho mazuri, limevaa masketi ya ndani, na—na vitu hivi vingine vyote wanavyovaa namna hiyo. Hakika, lilionekana ni la kiungwana, “Baba, Kasisi, Daktari, Baba *Nanii*.” Loo, jamani! Wangeweza kumweka “mbwa” halisi, mle.

<sup>81</sup> Lakini, mnaona, kilikuwa ni kitu chotara. Chotara! Mnaona, hakikuwa na Uhai wowote ndani yake. Wala hawawezi kurudi tena, hiyo ndiyo sababu kamwe hawainuki. Uamsho wa Kilutheri kamwe haukuinuka tena. Uamsho wa Wesley kamwe haukuinuka tena. Uamsho wa Kinazarayo haukuinuka tena. Wala uamsho wa Kipentekoste hautainuka tena. Kwa nini? Kwa maana mliuua. Mliuchanganya na ulimwengu, pamoja na wazo la Unikolai, hamkumwacha Roho Mtakatifu afanye apendavyo. Hiyo ni kweli. Mlilifanya kanisa chotara, wala haliwezi kujizaa tena. Unapolizalisha, unapata Wamethodisti zaidi; Wabaptisti wakizaa, wanapata Wabaptisti zaidi; Katoliki ikizaa, inapata Wakatoliki zaidi; utapata kitu kile kile unachoambua kutoka kwenye suke. Lakini hebu nikwambie jambo fulani; Roho Mtakatifu anaporudi, Yeye huleta kuzaliwa *upya* na Maisha *mapya*; uongofu. Ubatizo wa Roho; hurudisha Kanisa kwa nafsi yake tena, huweka Uhai mpya ndani yake.

<sup>82</sup> Mahindi chotara hayana uhai ndani yake. Uhai uliopo, uko tu karibu kwisha. Sasa, tunapata hilo katika Wakati ule wa Giza kule, “Kile kidogo ulicho nacho, kishikilie” Yeye alisema. Walikuwa wameubinya wote. Sasa, bali hautajizaa tena. Sasa, ninii...

<sup>83</sup> Lakini Mwili wa Yesu Kristo sio—sio dhehebu. Mwili wa Yesu Kristo ni Mwili wa kisiri, ni Mwili wa... katika Ufalme ambaao ni Ufalme wa kiroho uliowekwa duniani na Yesu Kristo akiwa ndiye Mfalme wa Ufalme huu, Kuhani Mkuu wa kutoa dhabihu kwa ajili ya wasafiri katika Ufalme huu. Yeye ni Nabii (Neno) anayehubiri ile Kweli na kuileta Nuru ya Mungu katika Ufalme huu; Naye ni Nabii, Kuhani, na Mfalme pia, katika

Ufalme huu. Basi tunaingiaje katika Ufalme huu? kwa dhehebu? kwa barua? kwa kupeana mikono? Bali “kwa Roho Mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja” ambao ni Mwili wa kisiri wa Yesu Kristo, nasi tumebatizwa mle, sio kwa maji, sio kwa kunyunyiziwa, sio kwa kumwagiliwa, sio kwa namna yoyote ya ubatizo wa maji, bali “kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja,” Wakorintho wa Kwanza 12. Naam, tunabatizwa katika Mwili huu kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, ndipo sisi si mali ya chochote ila Kristo. Wewe ni wa Kristo. Ni Ufalme wa kisiri wa Mungu uliowekwa, ambao tunaingia ndani Yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Napenda Hilo! Hmm!

Wapo watu karibu kila mahali,  
 Ambao mioyo yao inawaka moto  
 Kwa moto ulioshuka Pentekoste,  
 Uliowasafisha na kuwafanya safi;  
 Loo, unawaka moyoni mwangu sasa,  
 Loo, utukufu kwa Jina Lake!  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao, Haleluya!  
 Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
 Sasa nina furaha sana kwamba ninaweza  
 kusema mimi ni mmoja wao.

Ingawa watu hawa huenda wasijifunze  
 kuwa, (D.D.D. Ph.D. Mnaona.)...huenda  
 wasijifunze kuwa,  
 Wala kujivunia sifa za ulimwengu,  
 Wote wamepokea Pentekoste yao,  
 Wakabatizwa katika Jina la Yesu;  
 Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na kwa  
 upana,  
 nguvu Zake zingali ni zile zile,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao.

Wewe huna furaha? Naam, bwana. Mmoja wao tu. Hivyo tu.

<sup>84</sup> Ninakumbuka nikitembea kupitia Memphis, maskini yule mama mweusi aliyekiegemeza kichwa chake juu pale. Akasema, “Habari za asubuhi, kasisi.”

Nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?”

Akasema, “Bwana aliniambia, ‘Kasisi Wake anashuka kuja mtaani, atakuwa amevaa kofia ya hudhurungi, amebeba mkoba.’” Kasema, “Nilijua ulikuwa ni yeye nilipokuona ukija.” Mnaona? Loo, yeye alikuwa ni mmoja wao. Hiyo ni kweli! Loo, jinsi Mungu alivyo mwema!

<sup>85</sup> Sasa ninaamini jambo fulani...[Ndugu Branham anasoma muhtasari aliopewa—Mh.] “Yule msichana mdogo u—uliyemwombea, Jumapili usiku, kutoka Bedford, anadhaniwa amekufa. Hili haliwezi...Tafadhalii omba dua.” Msichana mdogo ambaye sisi...waliyemwombea hapa Jumapili usiku, kutoka Bedford, “ame—amekufa sasa hivi,” walisema. Hebu tuombe dua:

<sup>86</sup> Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba kwa namna fulani, kwa njia fulani, Bwana, maombi yetu na yasikiwe kwa ajili ya mtoto huyo. Tunakikabidhi maskini kiumbe hicho Kwako, Baba yetu Mungu. Pia tunawazia juu ya watu hao waliokuwa hapa na kusihii na kuomba dua kwa ajili ya msichana huyo mdogo. Ee Baba Mungu, ninaomba ya kwamba—ya kwamba ripoti hii isiwe ya kweli, Baba; hatujui, bali ninaomba ya kwamba utaturehemu na kutupa nguvu na kuruhusu maskini kiumbe hicho kifufuke na kuishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina. Bwana Yesu na aongeze baraka Zake.

<sup>87</sup> Sasa, kanisa. Sasa, jina la kanisa linahusishwa na asili ya tabia yake. Mlijua *Smirna* linamaanisha “uchungu”? Nanyi mnaona kila moja ya kanisa sasa, ni jina la kanisa lililo na uhusiano na tabia ya kanisa hilo. Ningeweza kusema jambo fulani hapa; lakini afadhalii nisiliseme, maana mngeenielewa vibaya. Mnaona?

<sup>88</sup> Jina lako linao, pia. Huenda usijue hilo, bali linao. Loo, naam. Unasema sasa, “Hiyo ni elimu ya tarakimu.” La, siyo. Wakati Yakobo alipozaliwa walimwita *Yakobo* ambalo maana yake ni “mtwaa mahali pa mwininge;” lakini alipopigana mwereka na malaika, Mungu alibadilisha jina lake likawa *Israeli*, “mtawala.” Hiyo ni kweli? Sauli alikuwa “Sauli wa Tarso,” mtu katili; lakini, alipomjia Yesu, aliitwa “Paulo.” Jina la Simoni lilikuwa “Simoni”; bali alipomjia Yesu, aliitwa *Petro*, “jiwe dogo.” Loo, naam, bwana. Ninii...Jina lako linahusika na kile ulicho...Lina ushawishi juu ya tabia yako.

<sup>89</sup> Nalo kanisa hili liliitwa Smirna kwa sababu lilikuwa linakufa. *Smirna* linamaanisha “uchungu.” Kwa maneno mengine, shina la uchungu lilikuwa likichipuka na lilikuwa likilisonga sana, lilikuwa likielekea kwenye manemane. Hiyo ndiyo wanaipaka miili, manemane, mnaona. Ilikuwa ni manemane, uvumba, kama mafuta. Manemane inatumiwa ku—kuipaka miili ikiisha kutiwa dawa isioze, na kadhalika. Inahusika na mauti, nalo kanisa lilikuwa linakufa.

<sup>90</sup> Na, loo, hivi hamwezi kuona, leo hii, enyi marafiki, ule uamsho mkuu wa Kipentekoste ambaao ulikuwa na Uhai miaka michache iliyopita, hivi hamwezi kuona unapakwa sasa manemane? Mnaona? Mafuta yale yale yaliyokuwa katika kanisa hili *hapa* yameshuka moja kwa moja na kulipaka hili *hapa*; likifa kwa sababu wanarudi kwenye matambara ya kikasisi, na kuvua

mavazi yao meupe, watakatifu. Maskini watu wale waliosimama huko nje, wakiwa na Roho Mtakatifu halisi, wakanena kwa lugha, na kumdhihirisha Mungu. Na, ndugu, walikuwa ni waaminifu na, “sufu yote na yadi moja upana.” Wa—walikuwa ni halisi kabisa, ungeweza kuwaaminia mahali popote. Sasa hujui utaamini nini wala utamwamini nani. Mnaona? Kuna jambo fulani lililotukia. Jambo fulani limetukia. Ni kitu gani? Wanapakwa manemane, ya uchungu. Wakiinuka. Mmoja . . .

<sup>91</sup> Ni kitu gani kiliusababisha? Mmoja aliingia, kulikuwa na ka—kanisa lililoitwa, la kwanza, lilikuwa ni Baraza Kuu. Ndipo wakaliita Assemblies of God. Kutoka kwa Assemblies of God likaja Church of God. Kutoka kwenye Church of God, ndipo wakaanza kuangalia ng'ambo ya pili, kasema, “Ninyi ni Assemblies.” Huyo mwininge kasema, “Ninyi ni Church of God.” Ndipo kutoka kwa hilo likaja United Pentecostal Church of God, juu ya hoja fulani. Halafu, muda si muda wajua, badala ya kuikubali Nuru na kutembea ndani Yake, mbona, walijiundia dhehebu mpaka wasingeweza kuikubali Nuru.

<sup>92</sup> Sasa, wakati u—ubatizo katika Jina la “Yesu Kristo” ulipoletwa badala ya “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” kwa Assemblies of God, walikuwa tayari wamejitia nanga kwa hiyo wasingeubadilisha. Nao wanajua ni Kweli! Nampa changamoto yejote wao aonyeshe kwamba si wa kweli kwa Biblia. Ni Ukweli mtupu. Lakini wafanye nini? Hawawezi kuuchukua. Unaona, wangevunja kanuni yao ya imani, hawawezi.

<sup>93</sup> Halafu Waumoja walifanya nini? Badala ya kuukubali na kuendelea, wakawa wagumu: “Mungu abarikiwe milele! Tunayo Nuru, nanyi hamna. Sisi ndio . . .” Walifanya nini? Wakaunda dhehebu. Huwezi kumwundia Mungu dhehebu. Mungu hata hana umbo, Biblia ilisema. La, hakuna kitu cha utaratibu kumhusu Mungu.

<sup>94</sup> Sasa, ndipo Waassemblies wakajaribu kumwundia dhehebu na kuwafanya . . . ninii yao . . . lao ndilo Kanisa ha—ha—halisi. Ndipo Waumoja wakaja, wakajaribu kuliundia lao dhehebu, nao walikuwa na “Nuru zaidi.” Basi walifanya nini? Walililipua kwa njia yao chungu ya kichoyo, ambayo walitumia. Badala ya kuutangaza kwa chumvi na utamu, walijaribu kumwondoa huyo nwininge kwenye ushirika, wasiwe na uhusiano wowote naye. Na hilo ndilo lililolisababisha. Ulikuwa umeenea, basi. Muda si muda mwajua, lingine likatokea, wakawa na *hili*, na sasa wakatengana. Mmoja akasema, “Yeye anakuja juu ya farasi mweupe.” Huyo mwininge anasema, “Yuaja juu ya wingu jeupe. Mungu abarikiwe, nitaunda dhehebu hapa.” Mnaona jinsi wafanyakavyo? Ikasambaza manemane—manemane. Ilifanya nini? Iliufungia udugu nje.

<sup>95</sup> Wanawake wengi, wanaume, usiku wa leo, katika Assemblies of God, wangetaka kuja na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo,

wakijua ya kwamba Huo ni Ukweli wa Mungu. Wangefukuzwa kama wangefanya hivyo.

<sup>96</sup> Na wengi Waumoja wa . . . Sasa, mimi si Waumoja. Siamini “umoja” katika ile njia wanayouamini. Siamini Yesu jinsi watakavyosema, “Yesu”; kuna Mayesu wengi sana. Ni *Bwana Yesu Kristo*. Hiyo ni kweli. Sasa, wala sininii . . . Ninaamini hilo tofauti na vile wanavyoamini. Wanabatiza katika jina la Yesu, katika jina la Yesu kwa kuongoka, ya kwamba “Kubatizwa (kuongoka) kunamleta Kristo kwako kwa ajili ya ubatizo wako wa maji.” Siamini hilo. Ninaamini kuongoka huja kwa Damu ya Yesu Kristo kupitia kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Ubatizo ni tendo tu la nje kwa kazi ya ndani ya kuzaliwa upya ambayo tayari imefanyika. Mnaona? Kwa hiyo, sikubaliani na jambo hilo. Hilo ni sawa, bali wote ni ndugu zangu.

<sup>97</sup> Wakati nilipoanza kama mhubiri wa Kibaptisti kwa mara ya kwanza, walikaribia wakasema, “Ndugu Branham, wewe njoo huku, tu—tu—tunalo na tulilileta hapa.”

<sup>98</sup> Nikasema, “Si hata mmoja wenu, ninasimama moja kwa moja katikati ya vikundi hivyo viwili na kusema, ‘Sisi ni ndugu!’” Sijali nini, sijali kama mtu ananipinga, hilo halileti chembe moja ya tofauti kwangu, ye ye angali ni ndugu yangu.

<sup>99</sup> Ninaye ndugu anayependa sambusa ya matofaa; mimi napenda ya cheri zaidi, bali sitamwondosha kwenye ushirika. Anaweza kula sambusa yake ya tofaa nami nile yangu ya cheri. Nami naweka *ute wa yai uliopigwa na sukari juu ya yangu*, kama haitaki, mbona, anaweza kuichukua. Mnajua hilo . . . Ni kitu gani? Vile vitu vilivyotwangwa wanavyoweka juu yake, mwajua, “*krimu iliyyotwangwa*.” Ninaipenda. Ninazeeka kupita kiasi sasa kuila, lakini ni ninii . . . Lakini mimi—mimi—mimi . . . Hiyo ndiyo ninayopenda. Kama ye ye haipendi, sio lazima aile. Hiyo ni sawa, nitaila yangu. Lakini angali ni ndugu yangu! Hiyo ni kweli.

<sup>100</sup> Na kwa hiyo na—napenda hilo, napenda ushirika. Lakini wakati tunapochora mistari namma hii, na kusema, “La, hili ni dhehebu *letu*,” wala hatutanyosha mkono na kupeana mikono na huyo mtu mwingine, na kusema, “Mungu abarikiwe, ndugu!” Jamani! Hapo ndipo unapoita ushirika. Usipofanya hivyo, unapata shina la uchungu kama tu Wasmirna walivyoupata kule nyuma, nawe unasababisha jambo lile lile. Vema, kwa hiyo jina lao lilikuwa “uchungu.”

<sup>101</sup> Wanikolai waliendelea kuwazima mpaka kwenye zile Nyakati za Giza. Wakati wa Luther uliletu hatua ya kwanza ya neema, Nuru kidogo ikaanza kuangaza. Ndipo akatokea baada ya hayo, akaja John Wesley pamoja na utakaso, nayo ikang’aa zaidi kidogo. Ndipo ukaja ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na Wapentekoste, ukiirudisha tena imani ya baba zao. Bali wasingeweza kuidumisha jinsi hiyo, hivyo basi iliwabidi

kuiundia dhehebu, ndipo wakaanza kurudi moja kwa moja katika Unikolai tena. Vile hasa Biblia ilivyosema wangefanya.

<sup>102</sup> Sasa, inanibidi kuangalia hapa ama nitaipata... wakati mwinci sana umechukuliwa. Hebu tukiendee kifungu cha pili, ama ninii... hicho kingekuwa ni kifungu cha 8, 9. Vema, sasa yale mateso, kifungu cha 9:

*Najau matendo yako, dhiki yako,... umaskini, (lakini u tajiri)... (Loo, jamani!)... mimi... (Sasa Yeye anazungumza na Kanisa sasa, Kanisa halisi, sio wengine; walichukia matendo hayo ya Wanikolai.) ... najau na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali wao ni Sinagogi la Shetani.*

<sup>103</sup> Sasa, walikuwa wakilalamika. Walikuwa maskini sana. Ninii... Walikuwa wamechukua yote waliyokuwa nayo. Walikuwa wamejenga kanisa lao dogo kama hili, na kwa kuwa walikuwa ni kundi dogo sana, walikuwa wamewasukuma nje, lile kanisa kubwa lilikuwa limefanya hivyo, wakalinyamazisha kabisa. Nalo likasema, "Ninajua. Ninajua inawabidi kukutana huko chini pembeni, mnakutana vichochoroni, ama mahali popote pengine mwezapo." (Nami nimekuwa kwenye mapango ya kuzikia ambamo wanalazimika kukutania; wanateremka chini ya ardhi na kukutana, na kadhalika mle.) "Ninajua dhiki zako, pia ninajua shida zako, na kadhalika namna hiyo, bali unafanywa tajiri kwa dhiki hizo." Loo, jamani! Niambie wakati wowote mateso yanapokuja juu ya Kanisa, hulipa nguvu. Sikuzote yanalipa Kanisa nguvu, katika mateso. "Ninajua dhiki zako, bali u tajiri." Kwa nini? "Umenishikilia Mimi; u tajiri. Bali dhiki zako hazikuudhi."

<sup>104</sup> Sasa, ninii... Mliona? Wanikolai walikuwa wamejipatia sinagogi sasa. Biblia ilisema hivyo hapa. Mliona hapa katika kifungu cha 9?

*Ambako... ambayo... nao sio, bali ni Sinagogi la Shetani.*

<sup>105</sup> Uh-huh, Kanisa la kweli lilikuwa limesukumiwa nje. Wanikolai walikuwa wamechukua mamlaka, na ninii... walikuwa wamewafukuza watu waliokuwa na Roho Mtakatifu, kwa hiyo basi ha—hawakuwa na haja nao. Endapo Smirna, huko Asia, ingalijua tu ya kwamba mambo... ya kwamba taji za wafia imani zingaliwangojea, wangalitetemeka. Mnaona? Sasa, kwa maneno mengine, kile... wakati unabii huu ulipoandikwa na kutumwa chini, nalo kanisa likaupata, nao wakaona walikuwa ndio watakaovaa taji ya wafia imani, mbona, wangeninii... mbona, lingewashtusha hata kufa. Walikuwa wakiutazamia wakati wowote. Haukuja katika wakati wao. Halafu labda baadhi yao walisema, "Vema, mwajua—mwajua, nawaambia, nabii huyo alikosea. Yohana alikosea, yeye—yeye... kwa maana halikutukia kwetu sisi hapa Smirna." Mbona, ilikuwa iwe ni

mamia ya miaka baadaye. Mnaona? Lakini Mungu anaposema lolote, halina budi kutimia.

<sup>106</sup> Hapo ndipo tunaizamisha imani yetu, papo hapo kwenye Neno la Mungu. Mungu hutimiza kila ahadi. Haidhuru... Huenda ukawazia itatendeka papa hapa, bali labda huo si wakati wa Mungu kwake kutukia. "Lakini Neno Langu halitanirudia bure, bali litatimiza kile lililokusudiwa." Mungu daima ataliheshimu Neno Lake, na kwa wakati Wake mwema litavuna.

<sup>107</sup> Kwa hiyo watu hawa walikuwa ndio, kanisa la kwanza, bali katika kanisa hilo kulikuwako na tabia ambazo zingetokea katika kanisa la Smirna baadaye. Sasa, ndipo walikuwa watavaa taji ya wafia imani, wengi wao walikuwa wauawe.

<sup>108</sup> Sasa hebu tuchukue ki—kifungu cha 10, tunaposoma hili:

*Usiogope mambo haya (Sinagogi la Shetani) yatakayokupata: tazama, huyo ibilisi atawatupa... yenu gerezani, ili mjaribiwe; na kwamba mtakuwa na dhiki siku kumi: Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*

<sup>109</sup> Loo, jamani! Waliambiwa wasiogope walipoitwa waifie dini ya—yao. Sasa, Dada Wood, popote ulipo, ninatumaini hili linakusaidia. Dada Wood alikuwa akiniambia, hivi majuzi, ilikuwa ni vigumu kwake kuelewa ni kwa nini wengine wangeokolewa na wengine wasingeokolewa. Wakati mwingine inakubidi kujuja... Mungu aliwaambia watu hawa, "Sasa, msiogope kuhusu hilo, maana Shetani atawatupa mle ndani, kwa sababu kwamba hawa Wanikolai waungwana ambao wamekuja na kuwasukuma ndani, kwa kuwa nitawaacha mfe kwa ajili ya huduma Yangu. Bali nitawapa taji ya Uzima kwenye siku ile." Kwa hiyo msinini...

<sup>110</sup> Sasa angalia, Yeye alisema... Sasa, kama ukiangalia tunaposoma kifungu hiki cha 10. Hebu nikisome tena:

*Usiogope mambo haya yatakayokupata: tazama, huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani, ili mjaribiwe; nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi: lakini uwe mwaminifu hata... (Je, mliona hilo halikuwa mpaka? Sio mpaka kufa, bali "hata" kufa. Mnalipata?) ... uwe mwaminifu hata kufa, ... (Mnaona? Nao walikuwa.)*

<sup>111</sup> Sasa Yeye alisema, Shetani... Hivi mliona yule ambaye Yeye—ambaye Yeye alimtaja kama yule aliyekuwa akifanya hivyo? Sasa, hili *sinagogi la Shetani* lilikuwa ni hao "Wanikolai." Tunajua hilo. Sivyo? Basi lilikuwa ni dhehebu, ukasisi uliokuwa ukiinuka ambao ungewafanya watu hawa kuteseka, ambalo lingewafanya watu hawa kuteseka, nao iliwabidi kuwa waaminifu kwa Injili *hata* kufa. Hivi mliona katika sherehe ya ndoa? sio mpaka mauti yatakapotutenganisha, bali "*hata*

mauti yatakapotutenganisha.” Mnaona? Sasa, *hata na mpaka ni tofauti*. Sasa, walikuwa wawe waaminifu kwa Kristo hata mauti. “Shukeni mwende moja kwa moja mautini nayo. Msiogope, kwa maana nitawapa taji.”

<sup>112</sup> Sasa hizi “siku kumi” wanazozungumzia hapa, siku kumi. Siku moja katika Biblia inawakilisha mwaka mmoja. Nazo hizi *siku kumi* zilikuwa ni ile “miaka kumi” ya utawala wa huyu D-i-o-c-l-e-a-t-i-o-n, Diocletian. Diocletian, ambaye alikuwa yule mfalme mkuu aliyetawala katika ninii ya mwisho... Vema, kuna wafalme wakuu kadhaa waliotawala Wakati wa Kanisa la Efeso. Na Nero, ninaamini, alikuwa ni mmoja. Naye huyu Diocletian hapa ndiye wa mwisho aliyetawala, katika miaka kumi ya mwisho, naye alikuwa ndiye mtesi mmwaga damu sana mionganii mwa wote. Yeye aliungana tu na kundi hili nao-nao wakawaua Wakristo kinyama, na kuwaua, wakawachoma moto, wa-wakafanya kila kitu, na ilikuwa ni miaka kumi ya mateso yenye umwagikaji mwingi sana wa damu kuliko mingine yote. Na wakati wake na utawala wake ulikuwa ni kutoka mwaka wa 302 hadi 312. Huo ulimalizia wakati wa Smirna, pamoja na kuingia kwa Konstantino. Naye aliingia mwaka wa 312, Konstantino aliingia. Huo ulikuwa ndio zile siku kumi za dhiki. Nazo zilianza na Nero na kuishia kwa Diocletian. Nayo yalianza na Nero, ilikuwa yapata mwaka wa 64 A.D. wakati Nero alipokichukua kitu cha enzi.

<sup>113</sup> Sasa, kifungu cha 11 ni ahadi. Sasa tutakichukua hiki kabla tu hatujafunga:

*Yeye aliye na sikio na alisikie hili neno ambalo Roho  
ayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapatikana na  
madhara ya mauti ya pili.*

<sup>114</sup> Sasa, sina budi kusema jambo fulani hapa, ya kwamba kusudi... Kama nikilifikiria, moyoni mwangu, wala nisiliseme, basi mimi ni mnafiki. Mnaona? Ninawatakeni muone jambo fulani hapa katika Maandiko, nami nafikiri lilikuwa ni moja ya mafumbo makubwa sana kwangu kwa muda mrefu mpaka nikapata kujua. Sasa, hebu tusome hilo kwa makini sana, sasa. Mnaona?

*Yeye aliye na sikio... (Kwa maneno mengine, “aliye na sikio kusikia”; mnaona, kwamba “yuko wazi kwa Roho.”) ...na alisikie hili neno ambalo Roho ayaambia makanisa;...*

Sasa mnaona, jambo lili hili, mateso haya na kila kitu kinakuja. Kila sehemu yake inapandana katika kila kanisa. Yale *makanisa*.

... *Roho anayaambia makanisa. Yeye ashindaye... (Katika kanisa lipi? La Efeso? Naam. Vema. Smirna? Naam, yote hayo.) ... Yeye ashindaye katika makanisa yote hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.*

<sup>115</sup> Yeye katika kanisa la Laodikia ashindaye nini? Awashindaye Wanikolai, ayashindaye mambo ya ulimwengu, ayashindaye haya madhehebu, aushindaye ukasisi huu, ashindaye kila kitu cha ulimwengu na kujitolea kabisa, na kumpenda Kristo. Hutapatikana na madhara ya mauti ya pili. Kwa nini? Yeye yuna Uzima wa Milele. Uzima wa Milele hauwezi kufa. Yesu alisema, "Yeye asikiaye kutoka kwangu yuna Uzima wa Milele, wala hatakuwa kamwe. Nitamfufua katika siku ya mwisho."

<sup>116</sup> Sasa, sasa, hapo... Sasa utaninii... Huenda kuna wengi wasiokubaliana na hili, bali ninawatakeni mfikirie kwa nguvu sana kabla hamjatoa maamuzi yenu. Mnaona? Nitasema jambo fulani sasa:

<sup>117</sup> Hiyo ndiyo sababu mimi siamini kuna kuzimu ya Milele. Haiwezekani kuwa na kuzimu ya Milele. Maana kama kuliwahi kuwa na kuzimu ya Milele, basi daima kulikuwako na kuzimu ya Milele, maana Milele... Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ndio sisi sote tunashindania. Na endapo utateketezwa daima na Milele, basi itakubidi kuwa na Uzima wa Milele ukiteketezwa, ndipo ingekuwa ni Mungu anayeteketeza. Huwezi kuwa na kuzimu ya Milele, na Biblia inasema dhahiri ya kwamba "kuzimu iliumbwaa." Na ikiwa imeumbwa, si ya Milele. Kitu chochote kilicho cha Milele kamwe hakikuumbwa; kilikuwako daima, ni cha Milele. Nayo Biblia inasema ya kwamba "Kuzimu iliumbiwa ibilisi pamoja na malaika wake." Kuzimu iliumbwaa, si ya Milele. Wala siamini ya kwamba mtu ataadhibiwa Milele.

<sup>118</sup> Ninaamini ya kwamba Biblia inasema dhahiri hapa, ya kwamba, "Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili." Sasa "mauti." Neno *mauti* linatokana na... ni hili, ni "utengano." Sasa, tunapotenganishwa na Mungu, katika dhambi, tumekufa tayari; Biblia ilisema hivyo. Tumefarakanishwa na Mungu, tumekatiliwa mbali, tumekufa katika dhambi na makosa; sisi ni wagoni kwa Mungu na dola Yake. Ndipo tunapompokea Mungu na tuna Uzima wa Milele, sisi ni watoto Wake na tu sehemu Yake.

<sup>119</sup> Mvulana wangu mdogo hapo, Joseph, ni sehemu yangu, haijalishi yale mimi... atakayopata kufanya. Yeye... Huenda mimi... Huenda asiwe... Kama nilikuwa mtu tajiri mno na nilikuwa na urithi mkuu sana, huenda akaninii, hata akirithi chochote; bali angali ni mwanangu, yeye ni sehemu yangu. Hakika, yeye ni sehemu yangu. Sasa, siwezi kumkana zaidi ya ninavyoweza kujikana mimi, kwa sababu yeye ni sehemu yangu. Uchunguzi wa damu ungeonyesha ya kwamba yeye ni wangu. Mnaona?

<sup>120</sup> Nao uchunguzi wa Damu unaonyesha kama wewe ni wa Mungu au sivyo. Mnaona? Ninyi ni watoto wa Mungu na mna Uzima wa Milele. Lakini nafsi itendayo dhambi, *nafsi* hiyo itatengwa. Hiyo ni kweli? Ndipo haitakuwako tena. Sasa

angalieni. Chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho, kwa sababu chochote kilichokuwa na mwanzo ni kiumbe. Lakini Mungu hakuumbwa, daima alikuwa ni Mungu. Hakuna mahali alipoumbiwa. Na jinsi pekee tunavyoweza kuwa na Uzima wa Milele ni kuwa sehemu ya uumbaji huo. Utukufu! Loo, laiti tungaliweza kuliona Hilo! Unaona vile Roho Mtakatifu anavyokufanya? Ni Roho Mtakatifu, Muumba Mwenyewe, Mungu Baba katika umbo la Roho, aitwaye “Roho Mtakatifu” kwa maana alikuwa juu ya mwili ulioitwa Yesu, Mwanawee; ambaye alimuumba Yesu, ule mwili, hiyo ndiyo sababu Huo ilibidi ufe. Mungu aliishi katika mwili huu wa kibinadamu, nayo seli ya damu ilivunjwa, nao Uhai uliotoka katika seli hiyo ya damu ukarudi.

<sup>121</sup> Hiyo ndiyo sababu ambayo mwabuduo wa kale wa Agano la Kale asingeondoka . . . aliondoka na hukumu ile ile aliyokuwa nayo wakati alipokuja. Lakini katika Agano Jipyä, Waebrania ilisema, kwamba, “Mwabuduo akiisha kutakaswa mara moja asingejiona tena kuwa ana dhambi.”

<sup>122</sup> Sasa, Agano la Kale; wao walimleta mwana-kondoo, akamlaza chini, akaweka mikono yake juu yake, mwabuduo; kuhani akamkata shingo, akahisi kutokwa na damu, na akasikia mlío wake. Naye akafa, na akauhisi maskini mwili wake ukishupaa, naye akafa. Alijua huyo alipaswa kuwa ni yeye; mwana-kondoo alipachukua mahali pake. Kuhani akachukua hiyo damu, akaiweka madhabahuni na—nao moshi ukapaa juu, nayo yalikuwa ni maombi ya msamaha wa mwabu- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . wala uhai wa mnyama huyo usingerudi juu ya mwanadamu na kuungana na roho ya kibinadamu, kwa sababu ni roho ya mnyama. Uhai wa mnyama na uhai wa mwanadamu, haingewezekana. Lakini wakati ninii . . . Hiyo ndiyo sababu alitoka akiwa na tamaa ile ile ya kutenda dhambi, jambo lile lile. Anaingia ndani kwa ajili ya kufanya uzinzi, na kutoa dhabihu yake, kisha anarudi akiwa na jambo lile lile niani mwake. Hiyo ni kweli.

<sup>123</sup> Lakini hapa wakati mwabuduo . . . Loo, enyi Kanisa la Mungu, msikose kupata hili! Mwabuduo, akiisha kumwendea Mwana wa Mungu mara moja kwa kweli na kwa imani anaiweka mikono yake juu Yake (Loo, jamani!), anaangalia pale usoni Mwake huku yale mate yakining’inia usoni Mwake, Damu ikitiririka usoni Mwake, anahisi ule uchungu wa “Mungu Wangu! Mungu Wangu! Mbona umeniacha?” Loo, ndugu, unapoona ni gharama ya jinsi gani iliyokufa kwa ajili yako, na kwamba Huyo alikuwa ni nani, Imanueli, Mungu akifa mahali pako.

<sup>124</sup> Basi ni kitu gani kinachotukia? Mwabuduo basi, hapo seli hiyo ya damu ilipovunjwa katika Mwana wa Mungu . . . Ni kitu gani kilichoifanya seli hiyo ya damu?

<sup>125</sup> Wewe ni nini? Wewe ni seli moja ndogo iliyotoka kwa baba yako. Mwanamke hana himoglobini. Mwa—mwanamke hutoa yai pekee; kiangulio, ye ye atambeba m—m—mtoto. Bali damu inatoka kwa mwanamume, hiyo ndiyo sababu m—mtoto huchukua jina la baba yake. Halafu, bali, mwanamke akiolewa na mwanamume, huchukua jina la mume, kwa ajili ya watoto; ye ye anakuwa kiangulio cha mtoto huyo ambaye atamzalia mwanamume huyo. Lakini kama nilivyosema: kuku anaweza kutaga yai, bali endapo hajawa na ndege wa kiume, halitaangulika.

<sup>126</sup> Hiyo ni, nilisema, hiyo ndiyo sababu leo hii tuna makanisa mengi sana ya kale, baridi, ya kawaida. Waliingia kwenye wazo hili la Unikolai, wakapata viota vilivyojaa mayai yaliyooza, wala kamwe hayataanguliwa kwa sababu hayana... Ungewenza kuwafanya chochote (kuwaita maaskofu, mashemasi, na chochote kile), kamwe hawataamini katika ishara kuwafuata waaminio, kwa sababu hawajawahi kuwa na Mwenzi wao, Yesu Kristo. Kama kamwe ukipata kurutubishwa na Mwenzi huyo wa nguvu za Mungu...

<sup>127</sup> Wakati seli hiyo ya damu ilipovunjwa pale Kalvari, na Uhai huo uliokuwa mle ndani, Yehova mdogo... Loo, linapaswa kuvutia sana!

<sup>128</sup> Mwajua, kila mtu anatafuta ishara. Sivyo? Kila mtu anasema, “Loo, nionyeshe ishara.” Myahudi alisema, “Unionyeshe ishara.”

<sup>129</sup> Hebu niwape ishara. Mungu aliwapa ishara wakati mmoja. Waliomba wapate ishara. Israeli iliomba ipewe ishara. Yeye alimwambia nabii, “Nitawapa ishara ya milele: bikira atachukua mimba. Bikira atachukua mimba naye atamzaa Mwana.” (Amina.) “Ataitwa *Immanueli*, ‘Mungu pamoja nasi.’” Ishara kuu sana iliyopata kutolewa.

<sup>130</sup> Wakati Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, alipoufanya mfumo wa juu. Hebu simama pale kwenye Mlima Palomar uangalie huko ng’ambo kwa hiyo darubini, nawe unaweza kuona miaka mia moja na ishirini ya uwazi wa nuru. Vunja hizo katika maili, na ng’ambo ya huo kungali kuna mwezi, na nyota, na ulimwengu, Naye alivumba vyote. Alivipulizia tu kutoka mikononi mwake, namna *hiyo*. Naam!

<sup>131</sup> Ndipo huyo Muumbaji mkuu akawa Mwokozi Wangu. Akashuka akaja kwenye seli ndogo ya Damu, sio kupitia kwa mwanadamu, bali akaja kibikira kwa mwanamke; ndipo akachukua chavua hii ndogo kutoka kwa mwanamke, akajitengenezea Mwenyewe nyumba ndogo na kuishi ndani. Loo, li—li—linapaswa kuvutia! Yehova! Yehova, juu ya lundo la samadi katika kibanda, akilia. Yehova, katika hori la nyasi kavu. Hiyo ndiyo ishara ya milele, baadhi ya hawa watu wenye kiburi! Yehova, Mungu, mtoto mchanga anayelia

(Haleluya!) katika zizi linalonuka vibaya. Halafu tunafikiri ati sisi ni mtu fulani, unainua pua yako juu; kama ingalinyesha, ingalikuzamisha; halafu unatembea ukifikiri wewe ni mtu fulani. Naye Yehova amelala zizini, juu ya lu—lundo la samadi, akilia kama maskini...mtoto yejote mchanga. Linapaswa kuvutia! Hiyo ni ishara. Mungu alisema, "Nitawapa ishara ya milele." Hiyo ni ishara halisi. Yehova, akicheza kama mvulana. Yehova! Yehova, akifanya kazi katika karakana, akipasua mbao kama seremala. Haleluya! Jamani, loo, jamani! Yehova, akiiosha miguu ya wavuvi. "Nitawapa ishara."

<sup>132</sup> "Loo, bali inatubidi kuwa na makasisi, mwajua, wenye majoho na mishipi yote, kola, na..." Mnaona? Loo!

<sup>133</sup> "Nitawapa ishara ya milele." Yehova, akisimama uani akiwa na mate usoni Mwake. Yehova, ameanikwa uchi, katika mwili, kati ya mbingu na nchi. Yeye alidharau aibu ya msalaba. Tuna sanamu Yake pale akiwa amezungushiwa kitambaa kidogo; hakika huyo ni mchongaji aliyefanya hivyo. Walimvua nguo akawa uchi, wakamtahayarisha! Loo, hilo kundi la wanafiki wakati saa hiyo itakapofika! Hii ni siku ya mwanadamu, siku ya Bwana inakuja. Yehova! Yehova, akifa, naam, hakuna kilichotukia. Yehova, akiomba, hakuna kilichotokea. Hmm. Hiyo ni kweli. Linapaswa kuvutia! Hiyo ni ishara ya milele. Hiyo ndiyo ishara ambayo watu wote wangejua. Ndipo akafa, Yehova akafa. Ndipo nchi ikaanza kutetemeka. Loo, jamani!

<sup>134</sup> Ndipo akafufuka kutoka kaburini na kupaa Juu. Yehova, akirudi katika mfano wa Roho Mtakatifu apate kuishi katika Kanisa Lake, mionganoni mwa watu Wake. Utukufu! Yehovah, akitembea kanisani, akiyatambua mawazo ya nia zao. Yehova, akiwaponya wagonjwa. Yehova, akinena kupitia midomo hata mtu huyo hawezi kujidhibiti. Yehova, akirudi katika Kiingereza na kuitafsiri. Ati mnataka ishara? Amina! Kwamba Yehova alishuka kwa kahaba, akamwinua, ambapo yeye ni ninii sana—yeye ni duni sana hata mbwa wasingemwangalia, na kumwosha akawa mweupe kama sufu na kumpa roho safi kama yungiyungi. Loo, jamani! Yehova, akimchukua mlevi aliyelala pale kichochoroni na mayai ya nzi kote kinywani mwake, na kumfanya aihubiri Injili...?...Damu ya Yesu Kristo hutusafisha!

<sup>135</sup> Wakati alipokuwa duniani, alienda kwenye mji duni kuliko yote uliokuwako, na kwa watu duni kuliko wote waliokuwako, nao wakampa jina duni kuliko yote lililokuwapo. Hiyo ni kweli. Walimfanyia mabaya zaidi, na kumwitia jina baya sana ambalo lingeweza kuitwa mtu, "Beelizebuli," ibilisi. Kilicho duni sana wangaliweza kumpa, wanadamu walimpa.

<sup>136</sup> Lakini Mungu alimwinua, Naye akampa Kiti cha Enzi kilicho juu sana hata ilimbidi kuangalia chini kuitazama Mbingu. Amina! Utukufu! Na akampa Jina lililo juu ya kila jina

linalotajwa Mbinguni na duniani, na jamii yote ya Mbinguni na duniani inaitwa jina Lake. Hivyo ndivyo mwanadamu alivyomwazia; hivyo ndivyo Mungu alivyomwazia. Ee Mungu, jalia mawazo yangu yawe kama Yako, Baba. Naam, bwana. Ee Jina la thamani!

<sup>137</sup> Sasa, “Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa Milele.” Sasa, kama kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, nawe unaupata na tunautafuta kwa Yesu Kristo, huo ni Uzima wa Mungu. Basi wakati ile seli ya Damu ilipovunjwa kwa Mwana wa Mungu, na yule Yehova mdogo ambaye alikuwa amewekwa ndani ya Mtu huyu anayeitwa Yesu (wakati ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili), na sasa wakati tunapoikubali *hiyo* Damu kwa ondoleo la dhambi zetu, *hiyo* roho ambayo haikuwa juu ya mwanadamu, bali juu ya Mungu... Utukufu! Biblia ilisema, “Damu ya Mungu.”

<sup>138</sup> Mtu fulani alisema, “Mnakumbuka, Yeye... Usiseme chochote kuhusu Wayahudi, maana Yeye alikuwa ni Myahudi.” Yeye hakuwa Myahudi. Hakuwa Myahudi wala Mmataifa, alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli. Alikuwa ni Damu iliyoumbwa. Mungu aliifanya maalum. Ilikuwa ni Yake Mwenyewe, na kuitia kwa *hiyo* Damu iliyoumbwa tunaikubali kama msamaha wetu kwa sababu Yeye alikuwa hayo mauti kwa ajili yetu. Hiyo seli ya Damu ikivunjika, humwachilia Roho huyo Mtakatifu apate kurudi kwetu, na sasa sisi ni wana na binti za Mungu kwa kuzaliwa kwa Roho. Ndipo Uzima uliokuwa ni wa Mungu, ambao haukuwa na mwanzo wala hautakuwa na mwisho, ni wangu na wako kwa neema ya Mungu katika Yesu Kristo. Haya basi.

<sup>139</sup> Sasa, “kuzimu,” tutarejea kwenye hilo kidogo. Nawaambia ya kwamba—ya kwamba hakuwezi kuwako na... Ninaamini katika kuzimu kunakowaka moto. Naam, bwana, Biblia ilisema hivyo, ziwa la moto. Sasa, lakini *hiyo* haiwezi kuwa ni ninii ya mile...haiwezi kuwa ni ya Milele. Ingwezekana... Biblia kamwe haisemi ni ya Milele, inasema kuzimu ya “dawamu.” Haisemi neno Milele, inasema kuzimu ya “dawamu.” Sasa, imewekwa tayari kwa ajili ya ibilisi na malaika wake; kuzimu ya dawamu, sio ya Milele. Sasa, baada...Hiyo nafsi huenda ikateswa kule kwa matendo yake kwa muda wa miaka milioni kumi, nijuavyo mimi. Sijui vile *dawanu* huenda ikawa machoni pa Mungu. Huenda ikawa ni kwa dakika tano, huenda ikawa kwa miaka milioni moja, huenda ikawa ni kwa miaka milioni kumi, bali wakati utakuwa ambapo *hiyo* nafsi itakoma kuwepo.

<sup>140</sup> Haya hapa yale Biblia iliyosema, mnaona. Mnaona:

... *Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.*

<sup>141</sup> Mauti ya kwanza ni kutengana na wapendwa wetu. Tunaenda katika Uwepo wa Mungu, kamwe si nje ya Uwepo

Wake. Mnaona? Sasa, kama kuna mauti ya pili, basi itabidi iwe ni kifo cha nafsi. Ndipo basi yeye aushindaye ulimwengu, ama ashindaye mambo yaliyo katika ulimwengu, yuna Uzima wa Milele wala hataguswa na mauti ya pili. Haya basi, Uzima wa Milele. Lakini mwe—mwenye dhambi... Biblia ilisema, "Mwanamke aishiye katika anasa amekufa angali hai." Hiyo ni kweli? "Nafsi itendayo dhambi, hakika itakufa." *Kufa* ni nini? "Kutenganishwa" kabisa, "hayuko tena." Mnaona? Sasa, imekatiliwa mbali, ni kweli. Imekatiliwa mbali, haiko tena. Itachukua muda gani kuichukua hiyo? Itaenda chini kupitia njia ile ile iliyokujia, na itafikia mahali ambapo hakitasalia kitu kwake. Itarudi tu kwenye kitu kile ilichofanyiziwa.

<sup>142</sup> Tungeweza kuchukua seli, na kuivunja seli mara moja, kwa seli nyiningine, mpaka ufikie kwenye ile seli ya kwanza; uivunje seli hiyo, ndipo una kemia ya damu; unaingia kwenye kemia mbalimbali za damu, na ndipo unafikia kwenye sehemu ndogo katika seli hiyo: hiyo ni uhai. Hawawezi kuupata huo. Hawajui lolote kuuhusu. Sasa, uhai huo hatimaye utafikia mahali ambapo haupo tena; hata kemikali ya uhai huo iwe ni nini, siamini una kemikali yoyote. Ungekuwa ni wa kiroho.

<sup>143</sup> Halafu basi, katika jambo hilo, hatimaye utatenganishwa kabisa na usiwepo tena. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, "Nafsi itendayo dhambi, itakufa." "Na hao washindao katika nyakati hizi za kanisa hapa hawatapatikana na madhara ya mauti *ya pili*." Mwili unakufa kwanza, nafsi inafuatia kufa wala haitakuwako tena. Mnaona? Hiyo ni... mnaamini hiyo ni Biblia inayosema hayo?

<sup>144</sup> Sasa kumbukeni, kama kuzimu ni ya Milele, basi Biblia imekosea iliposema "kuzimu iliumbwu." Halafu basi kama mtu atachomwa moto Milele, kuzimuni, basi ingembidi kuwa na Uzima wa Milele apate kuhisi, kuunguzwa. Hiyo ni kweli? Vema, kuna aina ngapi za Uzima wa Milele? Moja. Hiyo ni kweli. Uzima mmoja tu wa Milele.

<sup>145</sup> Sasa, usiondoke na kusema, "Ndugu Branham haamini katika kuzimu." Ndugu Branham kweli anaamini katika kuzimu. Biblia inafundisha kuzimu ipo. Hakika tu kama vile kulivyo na ma—mahali pa raha, kuna mahali pa—pa adhabu. Naye Mungu hakika ataifanya nafsi itendayo dhambi dhidi Yake iadhibiwe. Na kwa kumkataa Yesu Kristo kama Mwokozi wako, hakika utaadhibiwa kwa ajili yake. Lakini kutakuwako na wakati ambapo wewe hutakuwapo tena. Lakini kwamba itachukua miaka milioni ngapi kwako kurejea pale, sijui mimi. Lakini wakati fulani...

<sup>146</sup> Wewe ni kiumbe cha wakati mpaka utakapozaliwa mara ya pili, ndipo wewe ni kiumbe cha Milele. Na jinsi pekee unavyoweza kuupata ni kuwa na sehemu ya Mungu ndani yako, ikiwa ni Uzima wa Milele. Unaweza kuona hilo? Hakika.

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho  
ayaambia makanisa; . . .*

<sup>147</sup> Ninampenda. Nanyi je? Nina furaha sana kuwa na Uzima wa Milele. Hilo halinisumbui tena, kwa sababu kwamba tuna Uzima wa Milele sasa. Nami ninajua hilo, na ninatumaini ya kwamba kila mtu atakuwa na Huo, sisi sote.

<sup>148</sup> Ireneo, naam, nilikuwa na muhtasari hapa juu ya Ireneo, kuhusu, “kusoma historia hii.” Kwamba sababu ya Ireneo kuchaguliwa ni kwa sababu alikuwa na ishara za Kanisa la Kipentekoste (asili) zikimfuata.

<sup>149</sup> Sasa, kama Mungu . . . Ni wangapi wanaamini ya kwamba Kanisa lilianzia Pentekoste? Vema. Ni wangapi wanaamini ya kwamba Mungu aliliidhinisha Kanisa huko Pentekoste? Vema, bwana. Basi kama hilo lilikuwa ndilo Kanisa la kwanza la Mungu, na hilo ndilo Yeye aliliita “Kanisa,” na Yeye sasa ni Mzabibu, sisi ni matawi, kama Mzabibu huo ukiwahi kuzaa tawi lingine, litakuwa ni nini? Pentekoste. Naam! Sasa, labda si kwa jina. Sasa tunayo *majina* ya Pentekoste, lakini hayo si zaidi ya Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste. Hilo halimaanishi kitu, mnaona, hilo ni jina tu. Lakini mradi tu una Ujuzi wa Kipentekoste moyoni mwako, pentekoste nafsi mwako, unaokupa Uzima wa Milele, basi Mungu amekuahidi ya kwamba, “Hutapatikana na madhara ya mauti ya pili,” kwamba, una Uzima wa Milele na *huwezi* kuguswa na mauti ya pili. Unaona? Una ninii . . . wewe ni . . .

<sup>150</sup> “Usimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu.” Sasa, usimhuzunishe (kufanya mambo mabaya). Ukimhuzunisha, utajuta; maana Biblia ilisema, “Usimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeche mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Hiyo ni kweli? “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu.”

<sup>151</sup> Loo! Itakuwa ni siku ya ajabu, asubuhi moja, moja ya nyakati hizi. Kuwaonyesha ya kwamba ufuluo utakuwa ni wa dunia nzima, “Wawili watakuwa kondeni, nami nitamchukua mmoja; na wawili kitandani, nami nitamchukua mmoja.” Mnaona, itakuwa ni usiku sehemu moja, na mchana sehemu nyingine ya dunia; utakuwa ni ufuluo wa dunia nzima, huo Unyakuo. Parapanda ya Mungu italia, na kila moja la haya, la kanisa hili dogo *hapa, hapa, hapa*, na hata lile kundi dogo lililopitia *kule*, na kutokeea *hapa, hapa, hapa*.

<sup>152</sup> Wakati yule mwanamwali, yule mwanamwali wakati alipoona katika zamu ya saba . . . Sasa, mtakumbuka, kulikuwako na wanawali saba. Hiyo ni kweli? Ama, ninamaanisha, wanawali watano walitoka . . . Wanawali kumi walitoka kwenda kumlaki Bwana, watano walikuwa wenye busara na watano walikuwa wapumbavu. Hiyo ni kweli? Na sasa, katika zile zamu hata hivyo, kulikuwako na zamu saba.

Na mwishoni mwa zamu ya saba (wengine walilala kutoka kwa zamu *hii, hii, hii, hii*, na *ile...*), zamu ya saba, sauti ilitokea, “Tazama, Bwana-arusi yuaja, nendeni mkamlaki.” Nao wakaamka na kuzitengeneza taa zao. Na hawa wengine wote wakaamka kupitia *hapa*. Loo, huo si utakuwa ni wakati mzuri sana!

Loo, tulizoea kuimba wimbo mdogo:

Ni wakati mzuri sana kwako,  
Ni wakati mzuri jinsi gani kwangu;  
Kama sote tukijitayarisha kumlaki Yesu  
Mfalme wetu,  
Itakuwa ni wakati mzuri jinsi gani.

Hapa, hebu tuone kama tunaweza kuuimba huo:

Wakati mzuri sana kwako,  
Wakati mzuri sana kwangu;  
Kama sote tukijitayarisha kumlaki Yesu  
Mfalme wetu,  
Utakuwa ni wakati wa ajabu jinsi gani. (Huo si  
utakuwa ni mzuri sana?)

Loo, hivi si kutakuwa kuzuri sana kule,  
Pasipo na mizigo ya kubeba?  
Kuimba kwa furaha huku kengele za moyoni  
zikilia,  
Loo, hivi si kutakuwa kuzuri sana kule?

<sup>153</sup> Ni wangapi wenu wanaojua mtafika nyumbani? Ni wangapi wenu wanaojua mtatokea kwenye mlango ule? Hamjui. Ni wangapi wanaojua kama ukitoka nje utarudi tena? Huwezi kujua. Kwa hiyo usiache usiku huu ushindwe; usimkosee Mungu usiku huu, kwa kuwa huenda huu ukawa ndio usiku wa mwisho ambaio ungepata wakati ama nafasi. U nani wewe, hata hivyo? Ulitoka wapi? Unaenda wapi? Kitabu pekee ulimwenguni kinachowenza kukwambia kwamba ni nini, ni maskini Biblia hii hapa iliyobarikiwa. Na hiyo ndiyo Biblia tunayoiamini, huyo ndiye Mungu tunayemwamini.

<sup>154</sup> Na kama huko kwenye Bibi-arusi huyo, katika kundi hili dogo la walio wachache, *huku* chini kabisa leo ukibanwa kabisa na kanuni za imani na madhehebu, na kadhalika, i—i—iwapo huko ndani ya kundi hilo dogo... Sasa, haikubidi kujiunga na maskani hii, haikubidi kujiunga na chochote, inakubidi tu kuzaliwa katika Ufalme huo. Sasa, kama unataka ushirika wako katika Methodisti, Baptisti, Presbiteri, popote unapoutaka, hiyo ni juu yako. Unaona, wewe weka ushirika wako pamoja na mtu yeyote utakaye. Ila nitakwambia jambo moja: unapozaliwa mara ya pili, unajua, “ndege wa aina moja . . .” Jamani!

<sup>155</sup> Mtu fulani aliniuliza wakati mmoja, kasema, “Ndugu Branham, uliwaambia hao watu, ‘Rudini kwenye kanisa la Kimethodisti.’”

Nikasema, "Hakika. Acha wawatupe nje, nao hawana mahali pa kwenda." Kwa hiyo basi tutaona . . .

Hilo ni sawa, rudi kule, haitachukua muda mrefu sana, unaona. Haitachukua muda mrefu sana, watarudi moja kwa moja tena.

<sup>156</sup> Unajua, wakati mmoja katika . . . Nuhu . . . safina, mahali pa usalama, Nuhu, mafuriko makubwa yalikuja. Na hivyo basi Nuhu akamfungulia kunguru atoke safinani, naye akaenda tu akilia na kuangalia kila mahali. Mbona, aliridhika, maana alikuwa mla mizoga tangu mwanzo. Angeruka kutoka kwenye maskini mzoga mmoja uliokufa, na kulijaza tumbo lake kwa nyumbu huyu, kisha aende kule kwenye maskini kondoo hu-huyu na kulijaza tumbo naye, na kadhalika, ambako kulikuwa na kila namna ya mizoga mifu imesambaa kila mahali.

<sup>157</sup> Kwa hiyo kunguru ataketi tu chini pale na kulialia, "Jamani, nina yubile nikiwa peke yangu kabisa!" akilialia tu.

<sup>158</sup> Lakini wakati walipomfungulia maskini yule hua, alikuwa wa asili nytingine. Uvundo huo, yeze "asingeweza kuuvumilia. Hmm!" Mbona? Hua hana nyongo yoyote; ndiye ndege pekee asiyekuwa na nyongo. Asingeweza kuumeng'enya, kwa hiyo jambo pekee angaliweza kufanya ni kurudi moja kwa moja kwenye safina na kubisha mlango.

<sup>159</sup> Nenda tu mahali popote utakapo. Jambo pekee ninalokuomba ufanye ni uingie tu kwenye ule Ufalme, nami ninajua utakakokwenda. Hutaweza kuyavumilia tena, ndugu, utasema, "Nimevuka mstari wa utengano, nimeuacha ulimwengu huu nyuma." Naam, bwana. Hakika ndivyo ilivyo.

Loo, walikuwa wamekusanyika kwenye  
chumba cha juu,  
Wote wakiomba katika Jina Lake,  
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,  
Na nguvu za utumishi zikaja;  
Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo  
Atakufanyia yayo hayo,  
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
mimi ni mmoja wao. (Na wewe je?)

Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
Nina furaha sana kwamba ninaweza  
kusema . . . mmoja wao, Haleluya;  
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
mimi ni mmoja wao.

Ni wangapi wana furaha kwa ajili ya hiyo usiku wa leo? Loo, jamani!

Njoo, ndugu yangu, tafuta baraka hii  
 Itakayousafisha moyo wako kutokana na  
 dhambi,  
 Itakayofanya kengele za shangwe zianze kulia  
 Na itaendelea kuiwasha moto nafsi yako;  
 Loo, unawaka moyoni mwangu sasa,  
 Ee, Jina Lake litukuzwe,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza  
 kusema...mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza  
 kusema...mmoja wao, Haleluya;  
 Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao.

<sup>160</sup> Sasa wakati tukiimba kifungu hiki kingine, ninawatakeni mpeane mikono, kama mfanyakyo kila usiku, Wamethodisti wote, na Wabaptisti, na Wapresbiteri. Peaneni mikono mmoja na mwenzake, na hata mwe wa kirafiki vya kutosha kutafuna chingamu ya mmoja kwa mwingine, mkiweza. Sasa iweni wa kirafiki sana, sana, mkiwa wachangamfu wakati tukiimba:

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao;  
 Mmoja wao, mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao.

Ingawa huenda watu hawa wasielimike  
 wakawa,  
 Wala kujivunia sifa za ulimwengu,  
 Wote wamepokea Pentekoste yao,  
 Wakabatizwa katika Jina la Yesu;  
 Nao wanatangaza sasa, kwa mbali na kwa  
 upana,  
 Nguvu Zake zingali ni zile zile,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza  
 kusema...

Sasa hebu tuuimbe kweli:

Loo, mmoja wao, mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza  
 kusema...mmoja wao, Haleluya;  
 Mmoja wao, mmoja wao,  
 Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
 mimi ni mmoja wao.

<sup>161</sup> Ungekuwa radhi kuwa mfa imani kwa ajili Yake pamoja na Wasmirna? Kama ikifikia mahali ambapo ilikubidi kukabiliana na mauti ama kuikana, ungekabiliana nayo? Naam, bwana.

Ee Mungu, ingekuwa ni furaha. Naam, bwana. Hivyo ndivyo ninavyotaka kwenda, moja kwa moja mimbarani. Hiyo ni kweli. Nilifikiri niliipata nao walikuwa wataipata huko Ujerumani hapa sio muda mrefu uliopita. Loo, walikuwa wakitaka kunipiga risasi kwa darubini ya usiku, nao askari wa Kijerumani upesi wakanizunguka na kushikilia nyuma namna *hiyo*. Nikawazia, "Lingekuwa ni jambo zuri jinsi gani kumfia Bwana wangu papa hapa hudumanii." Loo, jamani! Ni—ni jambo zuri jinsi gani.

<sup>162</sup> Vema, hebu niwaimbie wimbo mdogo. Sivyo? Je, mna—mna wakati kwa ajili ya wimbo mdogo sana? Vema. Siwezi kuuimba, nitaunena. Loo, sikuzote nimetaka kuimba. Na baadhi ya siku hizi mtakapofika kwenye makazi yenu makubwa ya kupendeza huko Paradiso, huko chini kabisa mwishoni mwa msitu huko chini, ambako mimi na Russell Creech tutakuwa tukiwindia, mwajua. Huko chini kabisa mwishoni mwa misitu ile kuna kibanda kidogo huko ambacho Ndugu Neville huimba sifa zake, *Nijengee Kibanda Pembeni*, (Nilifikiri alikuwa akizungumza juu ya makazi yangu) . . . *katika Nchi ya Utukufu*. Moja ya asubuhi hizi mtakapotoka mwingle kwenye baraza lenu kubwa huko ng'ambo, na kuangalia huku na huku namna hiyo, huko mbali sana pembeni mkimsikia mtu fulani akiimba:

Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu,  
Iliyomwokoa mwovu kama mimi!

<sup>163</sup> Mseme, "Vema, Mungu abarikiwe, maskini Ndugu Branham alifaulu. Huyo hapo, ninamsikia amesimama kule sasa hivi, akiimba *Neema ya Ajabu*."

<sup>164</sup> Itakuwa ni neema ya ajabu iliyonileta kule. Hiyo ni kweli.

Lakini inatiririka damu, naam, (Hiyo ndiyo sababu ninahubiri Huu.) inatiririka damu,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu,  
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inaendelea kutiririka damu.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa Roho Mtakatifu,  
Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa kama mwanamume;  
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,  
Alifundisha ya kwamba Roho angewaokoa wanadamu na dhambi.

Walikuwako Petro na Paulo, na Yohana mtakatifu,  
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate kuangaza;

Waliichanganya damu yao, kama wale manabii  
wa kale,  
Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate  
kuhubiriwa kwa uaminifu.

Zipo nafsi chini ya madhabahu, (Wale wafia  
imani) wakilia, "Hata lini?"  
Bwana apate kuwaadhibu waliotenda mabaya;  
(Sikilizeni! Upesi!)  
Bali kutakuwako na wengine watakaotoa  
damu ya maisha yao  
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na  
mafuriko Yake yaliyomekundu sana.

Inatiririka damu, naam, inatiririka damu,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,  
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya  
Kweli,  
Injili hii ya Roho Mtakatifu inazidi kudondoka  
damu.

<sup>165</sup> Loo, kutakuwako na . . .

[Dada mmoja ananena kwa lugha nyingine, ndugu mmoja  
anatoa ufasiri. Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine,  
dada ananena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda.  
Ndugu mmoja anafasiri—Mh.] Utukufu. Amina. Amina. Hmm.  
Hmm. Utukufu. Amina. Naam.

<sup>166</sup> Amina. "Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo  
Roho ayaambia makanisa."

Nampenda . . .

Abuduni sasa, muone kile atakachofanya. Kama hujawahi  
kumpenda hapo awali, ungetaka kumpenda sasa? Waweza  
kusimama na kumtambua, kumchukua kama Mwokozi wako?

. . . mimi, (Mungu akubariki, ndugu.)  
Na kunu- . . .

Mtu mwingine atakayesimama, aseme, "Ninamtaka, sasa  
hivi, ninataka kumpenda"?

. . . -okovu  
. . . Kalvari.

Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki huko nyuma, ewe  
msichana.

Nampenda . . .

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho  
aliambia kanisa.

. . . alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>167</sup> Baba yetu wa Mbinguni, unapowaona hawa watatu wamesimama kwa miguu yao, Ee Mungu, nakuomba uwarehemu, Ee Uliye wa Milele, na uwape msamaha wa kila dhambi, na wokovu, Roho Mtakatifu maishani mwao, wasije wakaguswa na mauti ya pili. Wanatambua, Bwana, usiku wa leo, wanaposimama pale, kwamba—kwamba kuna kitu kinachokaribia. Roho Mtakatifu ametoa onyo. Kumwona Roho wa Mungu akishuka mionganoni mwa watu, kumwona akitenda kazi kulingana kabisa na Maandiko, jumbe tatu tu kisha kamalizia. Ee Mungu, ujumbe kwa kila mmoja.

<sup>168</sup> Sasa, Baba, tunakuomba Wewe uturehemu. Jalia Roho huyo wa thamani akae mionganoni mwetu. Jalia tumheshimu, Mungu; tujalie. Wachukue watu hawa chini ya ulinzi Wako, Baba, hao ni matunda ya Ujumbe huu usiku wa leo, na wa ujumbe kutoka kwa Roho Mtakatifu ulionenwa mionganoni mwetu. Nasi tunaomba, Baba Mungu, ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao siku zote za maisha yao. Pia jalia “katika ulimwengu usio na mwisho” jalia tukutane nao kule, wameokolewa kwa Damu na neema ya Kristo. Tunawatoa Kwako sasa, Baba, wajaze na Roho Wako Mtakatifu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>169</sup> Mungu awabariki, ndugu zangu. Yeyote aliye karibu na hao watu wanaosimama, Wakristo, wapeni mikono wanapoketi chini, wapeni...watakiensi baraka za Mungu.

<sup>170</sup> Mmeona vile Roho Mtakatifu alivyo mtiifu, jinsi anavyolifanya mwishoni kabisa? Mmeona? Biblia ilisema, “Na...hao wanaonena kwa lugha wawe wawili-wawili, ama sio...si zaidi ya watatu,” mnaona. Huo ujumbe sio wakati nilipokuwa nikizungumza, ni baada ya Huo kwisha. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa, kila mtu akiwa na uchaji sana na kusikiliza yale Roho asemayo. Ndipo ilikuwaje? Wenye dhambi walismama kutubu. Loo, wazia. Roho Mtakatifu Mwenyewe, sio kulifanya...hata kupitia Neno, amekuja na kudhihirisha.

<sup>171</sup> Ninawajua baadhi ya hawa watu wanaonena kwa lugha, ninawajua hao wote watatu walionena; nami na—najua wale waliotoa fasiri; ninajua maisha yao hayana dhambi mbele za Mungu. Ndugu Neville hapa, mchungaji wetu, mhudumu wa Kimethodisti; huyo ni mhudumu wa Kimethodisti, anayeketi hapa, alimpokea Roho Mtakatifu. Junie, huku, Ndugu Jackson, mhudumu mwininge wa Kimethodisti, alimpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli, akiwa na karama ya lugha na kufasiri.

<sup>172</sup> Na mnaona jinsi tumeliweka kanisa, kila mmoja ni mwenye kicho; Mungu akinena. Mnaona jinsi anavyonena kulingana na Biblia hasa; moja; ujumbe usipotokea vizuri tu, Yeye anaunena tena, bali hatanena zaidi ya mara tatu; mnaona, kulingana na Maandiko pale. Mnaona, Yeye atautoa ujumbe huo; kamwe hautatanishi, “kwa kuwa roho ya manabii humtii nabii.” Kila kitu kinasikiliza na ni kimya... .

<sup>173</sup> Sasa hivyo ndivyo kanisa linavyopaswa kuwa katika utaratibu. Sasa kwenu watu ambao huenda mko hapa kutoka nje, ambao mmenisikia nikilisema, hivyo ndivyo inavopaswa kuwa. Mnaona, ujumbe unatolewa. Mnaona matokeo yake? Inatendeka papo *hapo*. Jambo fulani hutukia, kama tu utambuzi ama roho nyininge yoyote. Yeye si ni wa ajabu? Loo, nina furaha sana kujua ya kwamba jambo lilo hilo lililoagizwa na Mtakatifu Paulo, papa *hapa*, halijafifia kufikia papa *hapa*. Lingali ni jambo lile lile. Loo, nina furaha sana ninaweza kusema mimi ni mmoja wao. Nawe je? Vema.

<sup>174</sup> Sasa, kesho usiku saa moja, tunauchukua wakati wa Laodikia, na huo ni wakati wa *kufunga ndoa*. Ninawatakeni mje kama mnaweza. Nilichelewa kidogo tu usiku wa leo, kwa sababu labda ya Roho Mtakatifu akinena na kadhalika. Ila bado kungali ni mapema, ni kama saa tatu na dakika ishirini tu. Na mara nydingi niko hapa saa nne ama tano, kwa hiyo hiyo ni mapema sana hapa. Kwa hiyo mnaufurahia u—u—ujumbe wa Bwana? Kweli mnaufurahia? Unailisha nafsi yenu.

<sup>175</sup> Mungu awabariki, watoto wangu. Mnajua, ninawapenda kwa moyo wangu wote. Na wakati mwengine wakati Roho anaponishika, hukata zote... Hivyo ndivyo Neno liliyvo, ni kali kama upanga wenye makali kuwili. Linakata likija, likienda, ndani, nje, kila njia. Lakini hilo ndilo linalotutahiri. Tohara hukatilia tu mbali nyama ya ziada, mambo tusiyopaswa kuwa nayo.

<sup>176</sup> Sasa, ninawatakeni muone. Je, mlimsikia Roho kwenye ufasiri usiku wa leo? "Komesheni ujinga huo!" Hilo hutahirisha. Iweni waaminifu! Sisi sote huenda kombo, bali Mungu anajua jinsi ya kutunyoa bamba. Sivyo? Yeye hakika anajua. Ninashukuru kwa ajili ya hilo. Nanyi je?

<sup>177</sup> Je, wewe ndiye maskini yule mpiga piano hapa? Sioni... Hivi Teddy...? Simwoni hapa mahali popote. Ni—ni huyu...? Vema, dada, tafadhalii. Huyo ni binti yako, Ndugu Daulton? Mkweo. Vema. Maskini msichana mzuri sana, ninashukuru sana kwamba wewe ni Mkristo. Vema, maskini wimbo wetu mzuri wa kupumukana ni upi? Hebu tujaribu mmoja, kabla tu hatujaimba, sasa. Hebu kidogo, dada, kabla hatujaimba *Peleka Jina la Yesu Kokote Uendako*.

<sup>178</sup> Ni wangapi wanaoujua *Msisahau Maombi Ya Familia*? Ni wangapi wanaoomba katika familia yenu, maombi yenu ya familia? Loo, hilo ni zuri. Hebu tuujaribu mara moja, kama tu siku za kale sasa:

Msisahau maombi ya familia,  
Yesu anataka kukutana nanyi pale;  
Yeye atachukua kila tatizo lenu,  
Loo, msisahau maombi ya familia.

Mnaupenda huo? Hebu tuujaribu tena:

Msisahau maombi ya familia,  
 Yesu anataka kukutana nanyi pale; (Mna  
 miadi, sasa.)  
 Yeye atachukua kila tatizo lenu,  
 Loo, msisahau maombi ya familia.

<sup>179</sup> [Dada mmoja anasema, “Ndugu Branham, naweza kusema jambo fulani?”—Mh.] Hakika unaweza, Dada. [Huyo dada anaanza kuzungumza. Sehemu tupu kwenye kanda.] Dada Nash, hilo ni zuri sana. Loo, kama mtaninii tu:

Kama tukiamini wala kamwe tusitilie shaka,  
 Yeye hakika atakufanikisha;  
 Mpelekee tu Bwana mzigo wako na uuache pale.

Iache pale, iache pale,  
 Mpelekee Bwana mzigo wako na uuache pale;  
 Kama tukiamini wala kamwe tusitilie shaka,  
 hakika atakufanikisha;  
 Mpelekee Bwana mizigo yako na uiache pale.

<sup>180</sup> Hivi hamzipendi hizo nyimbo za kale? Loo, ninaninii tu . . . Ninaamini hao watu walichukua kalamu na wakavuvuwa na Roho Mtakatifu kusoma hayo.

<sup>181</sup> Kama vile kipofu Fanny Crosby wakati hao watu wa duniani wa siku hiyo walipojaribu kumfanya aandike nyimbo za kilimwengu, kasema, “Mbona, utakuwa mwanamke tajiri.”

Akasema, “Nimeyaweka wakfu maisha yangu kwa Kristo, na kipaji changu chote.” Alikuwa kipofu, mwajua. Kasema, “Na—namwia Kristo maisha yangu na kila kitu.” Kasema . . .

<sup>182</sup> Ndipo kidogo wakaudhika naye kwa sababu alikataa nafasi kama hiyo. Yeye hakuza haki yake ya urithi kama Bw. Presley na hao wengine walivyofanya, bali a-alidumisha uadilifu wake. Kwa hiyo yeye—yeye . . . Wa—wakamwacha, kasema, “Basi utakapofika Mbinguni, kama kuna mahali kama hapo,” kasema, “kama uko jinsi ulivyo hapa, utakuwa kipofu.” Kasema, “Vipi kama wewe *ni* kipofu,” kasema, “utamjuaje?”

Akasema, “Nitamjua. Nitamjua.”

Kasema, “Vipi kama wewe *ni* kipofu? Vipi kama wewe *ni* kipofu?”

Akasema, “Nitagusa alama za misumari.” Ndipo akageuka, akaanza kurudi nyuma, akasema:

Nitamjua, nitamjua,  
 Na nitasimama karibu Naye nikiisha  
 kukombolewa;  
 Nitamjua, nitamjua  
 Kwa alama za misumari mkononi Mwake.

<sup>183</sup> Ee Yesu wangu, pamoja na hayo majeraha matano ya thamani, ukitokwa na damu kwa ajili yangu huko, ningewezaje kumkana Mtu huyo wa thamani? Acha nife, hebu niende... Hebu nипитие njia ya chochote kile, bali kamwe usiache nimkane huyo Mtu wa thamani anayetokwa na damu huko aliyekufa kwa ajili yangu. Naam.

<sup>184</sup> Na mnapoondoka usiku wa leo, unataka ku-: *Peleka Jina La Yesu Kokote Uendako*. Vema, dada. Naomba tusimame sasa, sote pamoja.

...Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na majonzi;  
Litakupa furaha na faraja,  
Peleka uendako.

Jina la thamani (Jina la thamani), Loo jinsi  
lilivyo tamu! (Loo jinsi lilivyo tamu)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu  
jinsi gani!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa tunapovinamisha vichwa vyetu, na kuimba pole pole:

Tukiliinamia Jina la Yesu,  
Tukisujudu miguuni Pake,  
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa  
Wafalme,  
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! (Tamu  
jinsi gani!)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.



*WAKATI WA KANISA LA SMIRNA* SWA60-1206  
(The Smyrnaean Church Age)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne jioni, tarehe 6 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)